# Nipashe

Jumanne Machi 5, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

0745 700710
LIKE & FOLLOW US

ISSN 0856 • Na. 0581606

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital




UKURASA 21

**CASEMIRO: MAN UTD IITUMIE CITY KAMA KIOO**



# 'Earphones' janga jipya

• **Bingwa** wa Muhimbili afichua wanaochangia vifaa hivyo wanavyoumia... *Endelea ukurasa 2*

**Uchunguzi** waanza tukio la mfungwa kunajisi mtoto nje ya gereza

UKURASA 3



**Profesa** Janabi asimulia mkasa kunyanyapaliwa kisa wembamba

UKURASA 5



**Wafungwa** 4,000 watoroka gerezani, wasalia 100; hali ya hatari yatangazwa

UKURASA 19



## Mabasi kufungwa kamera kufuatilia kila kitu safarini

UKURASA 3



UKURASA 2

Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi (wakati wa uhai wake), akimjulia hali Tundu Lissu hospitalini Nairobi, Kenya baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi jijini Dodoma Septemba 2017. **PICHA: MAKTABA**

## Lissu: Niliona utu wa Mwinyi alipokuja kuniona hospitalini

**MICHEZO** FEI TOTO, AZIZI KI VITANI LIGI KUU UK.24

KABWELA UK.7

# ‘Earphones’ janga jipya kwa usalama wa masikio

**Na Christina Mwakangale**

BINGWA wa Maradhi ya Masikio, Pua na Koo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) - Mloganzila, Dk. Jonas Ndasika, ametaja kuchangia spika za kuweka sikioni (earphone) ni chanzo cha maambukizi katika masikio.

Vilevile, amesema kusikiliza sauti kubwa kupitia vifaa hivyo pia kunaweza kusababisha upotevu wa usikivu kwa kuwa kunaathiri mishipa ya masikio.

Bingwa huyo alibainisha hayo jana katika mazungumzo na Kituo cha Habari cha TBC.

“Tunatoa elimu kuhusu matumizi ya ‘headphones’, ‘Earphone’ inaathiri moja kwa moja mishipa ya usikivu, kelele nyingi zinaweza kumweka mtu katika hatari ya kupoteza usikivu,” alionya bingwa huyo.

Alifafanua kuwa matumizi ya vifaa hivyo vya usikivu kwa muda mrefu ni hatari zaidi kwa kuwa husababisha unyevunyevu katika mfereji wa sikio.

Kwa wanaochangia vifaa hivyo, bingwa huyo alionya kuwa wanayaweka masikio yao katika hatari ya kushambuliwa na bakteria au fangasi kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.



“Kama unatumia vifaa hivyo, basi matumizi yawe sahihi, kama ni sauti, iwe sauti ya chini. Ili kuondoa hali ya kusababisha kupoteza usiku, usivae vifaa hivyo kwa muda mrefu.

“Unapochangia vifaa hivyo na mtu mwingine, unaweza kuhamisha maambukizi ya bakteria au fangasi kutoka kwa mtu huyo kuja kwako au kutoka kwako kwenda kwake,” alionya bingwa huyo.

Dk. Ndasika alisema sikio lina uwezo wa kujisafisha lenyewe na kitaalamu haishauriwi kusafisha kwa kutumia pamba za masikio zenye vijiti kwa kuwa kufanya hivyo kunasababisha nta laini inayolinda sikio kusukumwa ndani.

“Ukitumia pamba kusafisha masikio, maana yake uchafu uliomo ndani ya sikio hujirundika na kuwa mwingi, jambo ambalo linasababisha sikio kupoteza uwezo wake wa usikivu,” alifafanua.

Ingawa hakuna takwimu sahihi za idadi ya watu wanaotumia spika hizo za masikioni, sasa kunashuhudiwa watu wengi, hasa vijana wakitumia vifaa hivyo na hata kuazimana.



Katibu wa Bunge nchini ambaye ni Katibu wa Kanda ya Afrika ya Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola, Nenelwa Mwihambi, akizungumza na Katibu Mkuu wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Duniani, Stephen Twigg, alipomtembelea ofisini kwake bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

## Hitilafu Gridi ya Taifa chanzo mikoa mingi kukosa umeme

**Na Elizabeth Zaya**

BAADHI ya mikoa Tanzania Bara na Zanzibar jana ilikosa huduma ya umeme baada ya kutokea hitilafu katika Gridi ya Taifa.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano cha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Irene Marobe, aliiambia Nipashe jana kuwa baada ya kutokea hitilafu hiyo, mafundi walianza walichukua hatua za dharura kuhakikisha huduma hiyo inarejea haraka.

“Ni kweli hitilafu imetokea na kuathiri maeneo mengi ya nchi; Tanzania Bara na Zanzibar, lakini mafundi wamepambana tangu lilipotokea tatizo ili kurejesha huduma haraka,” alisema.

Alisisitiza utatuzi wa tatizo hilo usingechukua muda mrefu, akisema “tunaamini hata kesho (leo) haitafika litakuwa limetatuliwa kwa sababu mafundi wetu wanapambana sana kuhakikisha linatatuliwa ndani ya muda mfupi.

“Na tunavyozungumza sasa hivi (jana saa 11 jioni), kuna baadhi ya mikoa umeme umerejea ikiwamo Iringa na Dodoma.”

Hitilafu hiyo imetokea ikiwa ni takribani wiki moja tangu wananchi waanze kufurahia matunda ya Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP) ambao hivi karibuni mtambo wake namba tisa uliwashwa na kuingiza MW 235 kwenye Gridi ya Taifa na kupunguza mgawo wa umeme uliokuwa unatikisa nchini.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA ILALA
(JENGO LA WIZARA YA ARDHI – KIVUKONI)
MAOMBI MADOGO NAMBA 314 YA MWAKA 2023
TUJIJENGE TANZANIA LIMITED.................MWOMBAJI
DHIDI YA
SHARIFA OTHMAN KHALID..............MJIBU MAOMBI NA.1
RAMADHANI JUMA FIKIRINI...........MKIBU MAOMBI NA. 2
KUITWA SHAURINI
RAMADHANI JUMA FIKIRINI
POPOTE ULIPO
TUJIJENGE TANZANIA LIMITED
Amewasilisha shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala lililopo (jengo la wizara ya Ardhi – Kivukoni). Maombi hayo yamepangwa kutajwa tarehe 19/03/2024. Hivyo basi unatakiwa wewe mwenyewe au wakili wako kuleta kiapo kinzani “counter affidavit” ndani ya siku 7 kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa . vielelezo vyote vinavyohusu shauri tajwa vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Ilala. Endapo hamtatekeleza haya, maombi hayo yatasikilizwa upande mmoja na uamuzi/amri kutolewa.
Imetolewa na kutiwa muhuri wa Baraza leo tarehe 20 Mwezi Februari, Mwaka 2024.
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) – ILALA
DAR ES SALAAM

# Tundu Lissu: Niliona utu wa Mwinyi aliponifuata hospitalini Nairobi

**Na Maria Seme**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema Rais mstaafu, Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi alikuwa mkarimu na mwenye utu.

Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, amesema alithibitisha hilo pale Mzee Mwinyi alipokwenda Hospitali ya Nairobi, Kenya kumtembelea alipolazwa baada ya kupigwa risasi katika tukio la kikatili la Septemba 7, 2017.

“Mzee Mwinyi alikuwa mpole na mkarimu enzi za uhai wake. Nilipopigwa risasi Septemba 7, 2017 na kukimbizwa Nairobi kwa ajili ya matibabu, Mzee Mwinyi na Mama Sitti walikuja Hospitali ya Nairobi kunitakia kheri nipone haraka. Apumzike kwa amani ya milele!,” aliandika Lissu jana kwenye ukurasa wake rasmi wa mtandao wa X.

Lissu alipelekwa Hospitali ya Nairobi kwa dharura baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana waliommiminia risasi akiwa anajiandaa kushuka kwenye gari nyumbani kwake mjini Dodoma, akitokea bungeni alikoshiriki kikao cha mchana na kuchangia hoja.

**DK. SLAA**

Wakati Lissu akieleza hayo, aliyekuwa Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dk. Willibrod Slaa, amweelezea Hayati Mzee Mwinyi alivyoanzisha vita ya mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Dk. Slaa aliambia Nipashe jana kuwa anakumbuka Hayati Mzee Mwinyi alivyoanzisha mapambano hayo kwa kuunda Kamati ya Ukimwi ili kupambana na ugonjwa huo uliokuwa unatisha wakati wa uongozi wake.

Dk. Slaa alisema kuwa wakati huo ugonjwa huo ulikuwa umeshamiri nchini na pia wananchi waliougua ugonjwa huo waliogopa kujitokeza kupata huduma.

Alisema kuwa haikuwa rahisi kuwashawishi wananchi kupima kwa sababu waliogopa kunyanyapaliwa na kutengwa na jamii.

Kifo cha Mzee Mwinyi kilitangazwa Februari 29, mwaka huu na Rais Samia Suluhu Hassan, aliyesema kuwa Rais huyo wa awamu ya pili alifikwa na umauti akiwa katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam alikokuwa anapatiwa matibabu ya ugonjwa wa saratani ya mapafu.

Mwili wa Mzee Mwinyi ulizikwa katika Kijiji cha Mangapwani, Unguja Jumamosi iliyopita.

# Wanaougua magonjwa adimu wakosa fursa elimu

**Na Elizabeth Zaya**

WAZAZI wa watoto wanaougua magonjwa adimu, wameiomba serikali kuweka mtaala wa elimu utakaowawezesha wale wanaoumwa kama wao, kupata fursa ya elimu kama ilivyo kwa wengine.

Sharifa Mubaraka, mzazi wa mtoto anayeishi na ugonjwa huo, akizungumza katika maadhimisho ya siku hiyo yanayofanyika kila mwisho wa mwezi Februari, mzazi Sharifa Mubaraka, alisema mpaka sasa watoto wengi wanaougua ugonjwa huo wana shida ya fursa ya elimu. Alisema, sababu kuu ni kwamba wao wanahitaji uangalizi wa karibu zaidi, hususani kutoka kwa wazazi wao. Alifafanua: "Baadhi ya watoto au watu wanaougua ugonjwa huu ni wale wasio na uwezo wa kwenda kuchangamana na wengine."

Sharifa aliendelea kuwa: "Ni kwa sababu wengi wanakuwa wa nyumbani tu, wakihitaji uangalizi wa karibu, kwa hiyo tunaomba kundi hili litambuliwe hasa kwenye fursa ya elimu ili nao wapate haki yao hiyo."

Hivyo, Mzazi Sharifa, aliiomba serikali iangalie namna ya kupunguza saa za kazi kwa wazazi wanaolea watoto wenye ugonjwa huo, ili wapate muda wa kuwahudumia bila kuhofia kupoteza ajira zao.

Mmoja wa wanaoishi na ugonjwa huo aliyejitambulisha kwa jina moja na Irene, alisema kutokana na kukosekana kwa elimu ya kutosha juu ya ugonjwa huo, baadhi ya watu wanaouguza wenye maradhi hayo hukimbilia kwa waganga wa kienyeji wakidhani wamerogwa.

"Ni ugonjwa ambao umejificha sana. Wakati mwingine unakwenda kupimwa unakutwa ni mzima wakati tayari unaumwa na hii imechangia watu kuwa na imani potofu na kwenda kwa waganga kutafuta tiba mbadala wakati tiba pekee inapatikana hospitali," alisema Irene.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), Prof. Bruno Sunguya, aliahidi wataendelea kufanya utafiti kwa ajili ya kupata suluhisho ya ugonjwa huo.

"Tutaendelea kufanya tafiti ambazo zitachangia kupata suluhu ya matatizo, kujua namna bora ya kuishi na hali hiyo na kutoa mchango mkubsa kwenye jamii," alisema.

Prof. Sunguya, alifafanua kuwa, zaidi ya watu milioni 350 duniani wanaugua magonjwa adimu, huku asilimia tatu ya Watanzania wamo katika oridhja hiyo, wengi hawajitambui kama wanaugua ugonjwa huo.

Prof. Karimu Manji, Daktari Bingwa wa Afya ya Watoto, alisema na wao wamekuwa wakiungana na wengine duniani kusherehekea siku hiyo kila mwaka, kuhamasisha jamii itambue magonjwa hayo ili isiwanyanyapae watoto, wapate msaada unaohitajika.

# Mabasi kufungwa kamera kufuatilia kila kitu safarini

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema magari ya abiria ya masafa marefu, yatawekewa kamera zinazolenga kudhibiti usalama na uvunjifu wa sheria, vinavyofanywa na baadhi ya madereva.

Akizungumza katika mafunzo ya Kuwajengea Uwezo Waandishi wa Habari wilayani Kibaha, yaliyoandaliwa na LATRA, Mkurugenzi wa Udhibiti Usafiri wa Barabara, Johansen Kahatano, alisema, wanatarajia utaratibu huo uanze kabla ya Julai, mwaka huu.

"Sasa hivi tunaboresha kanuni zetu za leseni ya usafirishaji magari ya abiria, katika uboreshaji huo, tunataka magari ya masafa marefu yawe na kamera ndani yake ili kumwonyesha dereva, abiria waliomo ndani na nje ya gari.

"Lengo hapo ni kutaka kugundua vitendo vya uvunjifu wa sheria, lakini kuona namna dereva anavyoendesha gari yake," alisema Kahatano.

Alisema tayari wameshaanza maandalizi ya kanuni ambazo wanasubiri ziende kwa wadau, kabla ya kurejeshewa na baada ya kukamilisha maandalizi yake, watataka magari yote ya masafa marefu yanayokuja nchini yawe yamewekwa tayari kamera hizo.

"Tumeshakubaliana na watengenezaji wa magari, tumewaeleza mahitaji yetu kwamba kamera zinatakiwa ziwe za aina gani, ziwe ngapi, zikae sehemu gani.

"Utaratibu wa kuweka kamera hizo utasaidia kuimarisha usalama kwa watu wanaosafiri, kufahamu idadi ya wanaosafiri, wanakwenda wapi, usalama wenyewe wa gari na dereva wake na kuwa na uwezo wa kumuona anavyoendesha.

"Baada ya kufungwa kamera tutakuwa tuna uwezo wa kufuatilia na kuona kila kitu kinachoendelea ni kama vile ilivyo 'VTS' (mfumo wa kufuatilia safari ya basi), japokuwa hii yenyewe itakuwa kwa kuona kwa macho kila kitu kinachoendelea kwenye gari, alifafanua.

Kahatano alitaja faida nyingine ya kamera hizo, inasaidia kufahamu gari zinazozidisha abiria; kurahisisha uchunguzi wa ajali; kufahamu kilichotokea barabarani; hali ya dereva hadi kutokea kwa ajali na kupunguza vihatarishi vya ajali hizo.

"Hii tunaamini kwamba huenda ikawa sehemu ya tiba ya ajali mbalimbali ambazo zimekuwa zikitokea. Kwa hiyo pia itatusaidia na sisi kuona tufanye nini," alisema Kahatano.

Alisema tayari wameshafanya vikao na wadau na watoa huduma kuhusiana na mfumo huo. Katahano aliendelea:

"Watoa huduma tumefanya nao vikao wakiwamo waagizaji wa magari, wauzaji wenyewe na wao wakasema ni jambo ambalo lina faida kwa serikali.

"Pia na kwao wenyewe (wenye magari) kwamba huenda ikawasaidia kudhibiti baadhi ya vitu ikiwamo kuhakikisha wanapata kipato sahihi," alisema Kahatano aliendelea:

"Wanaona hiyo ni nzuri kwa sababu itawasaidia kujua idadi ya abiria wanaopanda kwenye gari na hivyo kupata kipato sahihi tofauti na sasa ambapo hakuna kamera, ambapo wakati mwingine wanasema hakuna abiria kumbe wamejaa, udanganyifu utapungua."



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, SACP Safia Jongo, akiwa na mmoja wa watoto wanaolelewa katika kituo cha yatima cha Neema House alipowatembelea kituoni hapo hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uchunguzi waanza mkasa mfungwa kunajisi mtoto

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, amelaani tukio la mtoto kunajisiwa na anayedaiwa mfungwa wa Gereza la Kalilankulukulu, akieleza kuwa tayari uchunguzi umeendelea ili hatua kali zichukuliwe.

Jana gazeti hili liliripoti kuhusu binti mwenye umri wa 14 kunajisiwa na anayedaiwa kuwa mfungwa wa gereza hilo lililoko Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, mkoani Katavi.

Mkuu wa Mkoa Mrindoko, akizungumza na waandishi wa habari jana, aliwatoa hofu wananchi wanaodhani suala hilo halitafanyiwa kazi.

Mrindoko alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Kaster Ngonyani kulishughulikia suala hilo kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na kuhakikisha sheria inachukua mkondo wake bila kujali aliyefanya kosa ni nani na anakotoka.

"Jambo la pili, ni lazima tutende haki kwa aliyetendwa ukatili huo, tumesikia mahojiano mafupi alichofanyiwa yule binti, kwa kweli ni jambo la kusikitisha na sisi serikali jambo hili tumelipokea kwa masikitiko makubwa.

"Niendelee kuwatoa wasiwasi wananchi, hakuna upendeleo wowote utakaofanyika, hakuna chochote kitakachofichwa, jambo hili litazingatia sheria kwa asilimia 100 na sisi tunalisimamia kikamilifu kuhakikisha haki inatendeka kwa kila mmoja.

"Kwa kuwa sheria ni msumeno, ninamwagiza tena Kamanda wa Polisi na Kamanda wa Magereza kuhakikisha sheria na usimamizi thabiti wa jambo hili.

"Anayetajwa na hata kama kuna mwingine anayehusika kwa namna moja au nyingine kufanya tukio hilo la kikatili, lazima wote watiwe mbaroni haraka iwezekanavyo na taratibu za kisheria ziendelee," aliagiza.

Aliongeza: "Matukio haya yapo, yanatokea katika jamii yetu ya Mkoa wa Katavi. Yanatokea kwa watoto wadogo, hata kwa watu wazima. Niombe sana jamii tufuate maadili ya kitanzania, masuala haya ya kubaka, kulawiti si utamaduni wala maadili ya kitanzania."

# ALI HASSAN MWINYI 1925 – 2024

## • Sekondari kata zilivyoanza mikononi mwake

**Na Peter Orwa**



SASA shule za kata zimemea kila mahali. Ni ushindi katika sekta ya elimu na mzunguko wake, utashi na ufahamu umesambaa.

Hata hivyo, kadri muda unavyosogea, kijamii si wote wanaojua historia kwa kina. Kimsingi, Tanzania kwa wastani wa miaka 20 tangu kupata uhuru, ilizama zaidi katika miradi ya elimu msingi na serikali hadi leo haijawahi kushusha pumzi katika hilo.

Baada ya uhuru, nchi ilitoka mara moja katika mfumo wa elimu wa madaraja matatu; wanufaika wakuu Wazungu, kufuatiwa na Waasia, kisha Waafrika nafasi kidogo.

Katika sera zake mwasisi wa nchi, Rais Julius Nyerere, alitoa kupaumbele kwa shule za msingi na kufuta ujinga kusoma na kuandika kwa wasiobahatika kwenda shule. Hiyo ndio ilihitajika, huku bajeti ya taifa ilidumu kipindi kirefu, wastani asilimia 25 ikizamia elimu.

Hadi kufika miaka 10 ya Uhuru, nchini kulikuwapo na maendeleo ya viwanda, ikiweka msukumo hitaji la wasomi zaidi ngazi ya sekondari na ufundi.

Lakini, bado idadi ya wanaoingia darasa la kwanza haikutosha, vilevile wasiojua kusoma na kuandika walikuwa wengi.

Rais Mwalimu Julius Nyerere, ikawa ni kikohozi kwake. Akawekeza zaidi katika elimu msingi na kufika mwaka 1974, kukashudiwa makubwa katika elimu.

Tanzania ilitangazwa na Umoja wa Mataifa kwa mafanikio makubwa kielimu Afrika, ikiwamo kufuta ujinga wakijua kusoma na kuandika.

Pia chama cha TANU kilipitisha Azimio la Musoma, mahsusi likihimiza elimu hasa ya msingi.

Tatu, mwaka wa kuundwa Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), sambamba na kuundwa mtaala mpya wa shule wa mwaka 1976, uliodumu miaka mingi.

Kichumi, Tanzania ikipiga hatua katika mapinduzi viwanda, mfano mwaka mmoja kabla, 1973, kukaanzishwa Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO).

Serikali, ikibuni mpango mpya wa miaka 20 kuanzia 1975, ulilenga viwanda vya kati na vikubwa. Hata hivyo ulisuasua kutokana na majanga, kama vita ya Uganda mwaka 1978 na kuvunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kitaifa kukaonekana ombwe la watumishi wahitajika wa elimu sekondari za ufundi, kilimo na biashara, ambazo ndizo mikondo ya mitaala.

Ndani ya miaka hiyo, kuanzia 1974 kisera kukawapo wadau shirikisi wa elimu nchini, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), ikabeba dhamana kujenga shule binfasi kama Kinondoni (Dar es Salaam), Jitengeni (Same), Kibohehe (Hai) na Jumuiya.

Vivyo hivyo, Jumuiya ya Wazazi ya TANU, ikaanzisha shule nyingi za ufundi kuanzia mwaka 1975 kama vile Bagamoyo Technical, Vituka (Dar es Salaam), Boza (Pangani), Lupata (Rungwe-Busokelo) na Ovada ya Manyoni.

**CHEMCHEM HALISI**

Kuanzia mwaka 1980/81 kukaonekana kuwa na hitaji kubwa la elimu sekondari, shule wahitimu hawazidi 5%. Serikali chini ya Mtendaji Mkuu, Waziri Mkuu Cleopa Msuya, ikabuni kufunguliwa fursa za sekondari binafsi.

Wazo likiwa na dhana wananchi katika maeneo yao kujipanga kujenga shule, ili kufungua nafasi zaidi za vijana wao kuiona sekondari.

Serikali ikawasaidia kuwaazima wakuu wanapatana nao, kwa mfumo uitwao "secondment" na kutokana na hali ngumu ya idadi ya walimu, wengi walikuwa wahitimu kidato cha sita.

Huku wakipewa mfano kuiga mikoa kama Kilimamjaro na Kagera zilizopiga hatua kwa kuwa na shule za wajihi huo, wenyeji wahitaji walitakiwa 'kuchangamkia fursa.'

Ni mwanzo wa ujenzi 'shule za kata' katika jamii. Baada tu ya kutangazwa, wilayani Rungwe kwa kutumia vigogo wake walioishi jijini Dar es Salaam, akiwamo Marehemu Jaji Yona Mwakasendo Eliy Anangisye, waliunda umoja na hatimaye kufika 1982 zikaonekana sekondari za wananchi; Mwakaleli na Lutengano.

Staili waliotumia ni nguvu ya wananchi na kile shule ikatafutiwa udhamini wa taasisi za dini, mathalani Mwakaleli (KKKT) na Lutengano (Morovian), vijiji vikapewa wajibu wa kifyatua matofali na madarasa waliopewa, wabebaji kutoka kijijini wanakijiji na wanafunzi.

Mwaka 1984 zikaonekana Ndembela (Sabato) mjini Tukuyu na nyingine ya Kipoke, iliyoko Kiwira chini ya Kanisa la Kibaptisti.

Kwa kipindi hicho, wilayani Njombe kasi hiyo hiyo nayo ikianzaa sekondari za Mpechi na Mtwango. Mfumo wa 'sekondari kata' ukaoleta hamasa na kumea kitaifa.

> **Mwaka 2008, pia Kikwete akabuni Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM), ambao una 'sapoti' kubwa ya Rais George Bush wa Marekani, aliyezuru nchini wakati huo.**

**MFUMO KUINGIA SERIKALINI**

Wastani wa miaka saba baadaye tangu kuanza mfumo huo, Mwalimu Nyerere kishang'atuka na Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi akiwa madarakani awamu ya kwanza, ndio ukawa mwanzo wa wazo hilo serikali.

Nchi ikiwa katika mageuzi makubwa kuelekea huria, kukawapo mahitaji zaidi wahitimu sekondari. Mwaka 1987, aliyekuwa Mbunge wa Kisarawe na Waziri wa Elimu, Prof. Kighoma Malima, akamuuzia wazo Rais Mwinyi, kuanzishwa Shule ya Sekondari ya Serikali kwa nguvu za umma, Kata ya Maneromango, Kisarawe Pwani.

Prof. Malima, akapigania jimbo lake akitumia pia hisani binafsi, wakati huo Mkuranga na Kisarawe ilikuwa wilaya moja na shule pekee ikiwa Minaki, iliyochukua pia wanafunzi wa mikoa tofauti.

Hadi kufika Julai 1988, Shule ya Sekondari Maneromango, ikazinduliwa kwa nguvu ya wananchi na wanafunzi wakawa wanaotoka mitaa ya mbali walipanga majumbani, wanaochukuliwa ni watokao Kisarawe na Mkuranga.

Ilileta mvuto, kundi kubwa lilikimbilia Kisarawe kurudia elimu msingi, kuvizia kufaulu wajiunge na Maneromango, ikizingatiwa kulikuwapo mwamko duni, wapo waliofuaulu Kisarawe lakini hawakujiunga Maneromango kukerwa na kwenda kupanga.

Mzee Mwinyi hakufanikiwa kuwekeza zaidi katika shule hizo, ikizingatiwa alielemewa na yaliyomgharimu ya mageuzi ya kimfumo, mfumuko mkubwa wa bei kufika 23%; kisiasa fukuto kubwa la mageuzi lililomwelemea kuanzia miaka ya 1990.

Mwaka 1995, Mzee Mwinyi alistaafu akamwachia Hayati Benjamin Mkapa. Hata hivyo, kabla ya kustaafu akaacha mageuzi ya ndoto yake kielimu, kubadili maslahi ya wasomi vyuo vikuu, akipanua Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pia kuanzishwa Chuo Kikuu Huria.

Mkapa akaanza kazi akitumia ushauri wa Mkuu wa Shule wa zamani aliyekwea kuwa Waziri wa Elimu, Jackson Makweta, aliyeitaka serikali kueneza aina ya shule za Maneromango kitaifa.

Rais Mkapa akalitekeleza, kupitia wakala wake mkuu, Waziri wa Elimu na Ufundi wakati huo, Mzee Joseph Mungai, aliyezunguka kitaifa kuwahamasisha ujenzi wa sekondari kwa nguvu za wananchi.

Kwa mujibu wa Mungai, akinukuliwa na chombo kimoja, Machi 2015, yeye, Rais Mkapa na Waziri Mkuu, Frederick Sumaye, wakausimamia mradi kama timu, hadi kuaanza kumea shule hizo za kata.

Pia kisera ilikuwa ajenda zake muhimu Rais Mkapa, alivyoanza na ubunifu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Elimu Msingi (MMEM), pia Mpango wa Maendeleo ya Elimu Sekondari (MMES), kuimarisha miundombinu, samani, idadi ya wanafunzi na tija darasani.

Kufika mwaka 2005 Mkapa anaondoka madarakani katika baadhi ya maeneo kulikuwapo shule zinamea na kwingine kukisuasua.

Hapo naye Naye Rais Jakaya Kikwete, akaingia akiendeleza ajenda hiyo ya elimu ya sekondari, pia elimu na afya alipobuni Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM).

Akihojiwa na mtangazaji wa Marekani, Tshaka Sally, katika kipindi cha Straight Talk Africa, Ikulu Dar es Saalam, Rais Kikwete akiwa na siku chache madarakani, akafafanua kwa kina alivyopania kukamilisha mradi wa sekondari.

Kikwete alianza kupangua wakuu wa mikoa na kubaki saba, akitoa angalizo kwa waliobaki akiwamo Yusuph Makamba, Dar es Salaam, tija yao ingeangaliwa na ukamilishaji miradi ya sekondari kata. Walipewa miezi saba ya kuikamilisha.

Hapo pakashuhudiwa kazi ya kuheshimika ya Hayati Waziri Mkuu Edward Lowassa, tangu Desemba 2005, akizunguka nchi nzima kuhangaikia miradi hiyo na daima hakupumzika hadi anaondoka madarakani, mapema 2008.

Kikwete, akamwachia jukumu mrithi wa Lowassa Mizengo Pinda, ambako akawapa majina na kuwapenda wanafunzi wake 'watoto wa mkulima'. Kuboresha tija ya wataalamu, Rais Kikwete akaviagiza vyuo vikuu vyote nchini kuwa na vitivo vya elimu, kupata walima zaidi kitafa, ikiwamo hata Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), huku wanasomea stadi hiyo walipata upendeleo maalum.

Zaidi 'mtaani', Rais Kikwete akaonekana katika miradi ya barabara iliyofungua mikoa ya kati na Kanda ya Ziwa, hadi Kigoma, vilevile Masasi Mtwara, hadi Tunduru, kufika Namtumbo mkoani Ruvuma.

Mwaka 2008, pia Kikwete akabuni Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM), ambao una 'sapoti' kubwa ya Rais George Bush wa Marekani, aliyezuru nchini wakati huo.

Hapo ndipo ikakamilika simulizi za kuzaliwa sekondari za kata, hata ikihamia katika ufanisi kitaaluma na kuimarika kwa kufikiwa, mahali kusikofikiwa nchini.

## HABARI KITAIFA

# Janabi aonya unyanyapaa dhidi ya wembamba

Na Christina Mwakangale

PROFESA Mohamed Janabi amesema mtu kuwa mwembamba haina maana kwamba ni mgonjwa, akionya unyanyapaa dhidi ya kundi hilo ambalo yeye ni sehemu yake.

Mkurugenzi Mtendaji huyo wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa Mradi wa Afua ya Mfumo Jumuishi hospitalini huko.

Ni mradi unaofadhiliwa na Bill & Melinda Gates, ukilenga kuboresha na kuongeza mitaala inayofaa kwenye masomo yanayohusu afya katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

Mradi huo wa miaka mitatu unaotarajiwa kugharimu Sh. bilioni 2.347, pia unalenga kupinga unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU).

Katika uzinduzi huo, Prof. Mohamed Janabi, alisema unyanyapaa upo hata miongoni mwa WAVIU, akieleza alivyoshuhudia hali hiyo wakati anatoa matibabu kwa kundi hilo.

Alisema kuwa alipokuwa anatoa matibabu kwao, wengi wao walimwona anafaa kuwatibu, wakiwakataa madaktari wengi kutokana na yeye (Janabi) kuwa mwembamba, hivyo kudhani naye huenda anaishi na VVU.

"Kilichonisikitisha, kwanini wagonjwa wengi wanaletwa kwangu pale 'emergency' (jengo la dharura) wakati huo ugonjwa huu ndio unashamiri nchini.

"Na dhana kuu ya jamii ilikuwa miongoni mwa wanaougua ni watu waliokonda au wembamba. Na mimi wakati huo nilikuwa mwembamba hasa.

"Nikavumilia ila siku nikamwuliza muuguzi mkuu 'mbona wagonjwa wengi mnawapangia kwangu?' Akasema wagonjwa wenyewe wanasema 'wewe ni mwathirika mwenzao, wanakuwa na faraja zaidi ukiwatibu wewe'," alisema Prof. Janabi.

Alisema unyanyapaa umeendelea kuwa tatizo la duniani licha ya kuwapo lengo la kutokomeza VVU na UKIMWI kufikia mwaka 2030.

"Mfano mwingine ni wa mwaka 2006, nikiwa Daktari Mkuu JKCI (Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete), tulishauriana 'kwanini tusiende kupima hadharani sisi viongozi ili kuhamasisha wengine?' Wote tulipima na Rais wakati huo na mkewe walifika.

"Tukaona takwimu zimeongezeka, waliojitokeza kupima kwa siku ni watu 70 na mwaka ule Tanzania ilikuwa na takwimu za idadi kubwa ya walioambukizwa VVU," alisema Prof. Janabi.

Alisema jamii inapaswa kuendelea kuhamasika na kujitokeza kupima afya ili kufikia malengo ya dunia ya 95:95:95, akisema ripoti zinasema nchi kama vile Botswana, Eswatini, Zimbabwe zimefikia 95:95:95. Kwa Tanzania changamoto ni katika asilimia 95 ya kwanza ya kutambua wanaougua.

"Kisukari au VVU? Siku zote huwa ninawauliza wanafunzi wangu kwamba kati ya hayo magonjwa ukiwekewa mezani utachagua nini?

"Kwa sababu ukibainika una VVU utaanza tiba na masharti ukifuata utaishi, ila kisukari kuna wakati hakisikii chakula, masharti wala dawa, ninajua kama mtaalamu.

"MNH kwa kushirikiana na MUHAS tumeanzisha afua ya miaka mitatu ambayo inalenga kupunguza unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya WAVIU, hasa katika maeneo wanayopokea huduma za afya, ikiwamo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili," alisema.

Prof. Janabi alisema mradi huo utatekelezwa katika nchi tatu ambazo ni Tanzania kupitia taasisi tajwa, Zambia kupitia Taasisi ya ZAMBART na Ghana kupitia Taasisi ya Educational Assessment and Research Centre (EARC) na washauri wao Research and Triangle Institute International (RTI) kutoka Marekani.

Mradi huo utahusisha kuboresha mitaala sita ya vyuo vya afya vya kati nchini pamoja na kuboresha mitaala ya afua ya mfumo jumuishi kwa watumishi walio kwenye vituo vya afya.

Sambamba na uboreshaji wa mitaala, mradi utahusisha mafunzo kwa asilimia 70 ya watumishi walio katika vituo vya afya pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya matokeo yatokanayo na afua hiyo.

Mgeni rasmi kati uzinduzi wa mradi huo, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, katika hotuba yake, iliyosomwa na Mkuu wa Programu kutoka Wizara ya Afya, Dk. Catherine Joachim, alisema

"Mradi huu hapa Muhimbili ni fursa ya kuwaleta pamoja wadau mbalimbali nchini pamoja na kuongeza uelewa kuhusu mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU.

"Ripoti ya kimataifa iitwayo 'Njia ya Kumaliza UKIMWI' inaonesha kuwa kumaliza UKIMWI ni uamuzi wa kisiasa, kifedha na nchi pamoja na viongozi wanaofuata njia hizo tayari wameshaona matokeo makubwa."

## Waliorejea shuleni baada ya kujifungua wapatiwa vifaa

Na Boniface Gideon, TANGA

KANISA la Mennonite Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Huduma Yangu Furaha Yangu (HYFY) wametoa msaada wa vifaa vya shule kwa wanafunzi 16 wa shule za awali, msingi na sekondari.

Miongoni mwa walionufaika na msaada huo ni mabinti waliorejea shuleni baada ya kukatisha masomo yao kutokana na kupata ujauzito.

Jana katika Kanisa la Mennonite Pongwe wakati wa kukabidhi msaada huo unaojumuisha sare za shule, madaftari, kalamu na viatu, Meneja Mipango wa shirika hilo, Magesa Wambura alisema kuwa mpaka sasa wameshawafikia wanafunzi zaidi ya 200 wanaotoka kwenye mazingira magumu na kuwasaidia misaada mbalimbali ili waendelee na masomo yao.

"Mpaka sasa tumeshawafikia wanafunzi zaidi ya 200 katika mikoa ya Tanga na Arusha, mpango wetu ni kuendelea kuwafikia watoto wengi zaidi.

"Tunawasaidia pia mabinti waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali zikiwamo mimba za utotoni, tunachokifanya ni kuwarudisha masomoni na kuwasaidia kila kitu mpaka watimize ndoto zao walizojiwekea," alisema Magesa.

Alisema moja ya vyanzo vikubwa vya watoto kukatisha masomo ni umaskini ambao husababisha mabinti kupata ujauzito kwa kudanganywa kwa vitu vidogovidogo. Sababu nyingine ni wazazi kushindwa kutimiza wajibu wao.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kinamama nchini waondolewe vikwazo hivi, wang'are kisiasa

**TOLEO** letu la jana lilikuwa na habari kuhusu madhila yaliyokumba wanawake waliojitokeza kuwania nafasi katika Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa uliopita.

Baadhi yao mbali na kueleza yaliyowasibu wakati wa mchakato wa uchaguzi, walishauri vyama vya siasa vifanye haraka maboresho ya sheria jumuisha suala la jinsia.

Madhila dhidi ya kundi hilo yanajumuisha kuombwa fedha, rushwa ya ngono, kudhalilishwa, kuambiwa nafasi wanazowania ni kwa ajili ya wanaume na kutoaminiwa na jamii husika, hali inayopunguza ushiriki wa wanawake kwenye siasa.

Pia wameeleza rushwa ya fedha, vitu na ngono ilivyokithiri katika vyama vya siasa huku mmoja akiweka wazi alilazimika kuuza gari lake ili ateuliwe kuwania udiwani.

Baadhi ya wanawake pia wameeleza kuwa katika uchaguzi uliopita (mwaka 2020) walijitosa kuwania nafasi mbalimbali, lakini majina yao 'yalikatwa' kutokana na sababu mbalimbali, mmoja wao akidai jina lake 'lilikatwa' kwa kuwa hajui kusoma na kuandika ilhali ni msomi na mkufunzi wa chuo kikuu.

Ni vikwazo ambavyo wamevitaja kuchangia kuwakatisha tamaa na hivyo kurudisha nyuma jitihada za kufikia usawa wa kijinsia, ambayo ni ajenda namba tano ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Nipashe, tukiwa wadau katika kuchochea utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, tunaona kuna haja wadau wote wa uchaguzi kuwajibika kuhakikisha kundi hili haliachwi nyuma katika uchaguzi unaofuata.

Ikirejewa hali ilivyo, Mkoa wa Dar es Salaam una wenyeviti 564. Kati yao, 64 ni wanawake na wawili wanakaimu. Manispaa ya Ubungo ina wenyeviti 90 (wanawake watano); Ilala inao 159 (wanawake 28), Temeke ina wenyeviti 142 (wanawake 12), Kigamboni inao 67 (wanawake wanne) na Kinondoni 106 (wanawake 18).

Nipashe tunaungana na wanawake na wadau wengine wanaotaka mfumo wa uchaguzi urekebishwe ili kutoa nafasi kwa kundi hili lililoachwa nyuma katika uongozi.

Udhalilishaji kingono na kutowapa nafasi wanawake kushiriki kuchaguliwa kuwa viongozi wakati wa uchaguzi si tu ni ukiukwaji wa sheria na haki za wanawake, bali pia ni kwenda kinyume cha mikataba ya kimataifa ambayo serikali imeshatia saini kuiridhia.

Tunatambua Serikali ya Tanzania imeshatia saini na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa Mwaka 1979 unaoelekeza kuondoa aina zote za ubaguzi na uonevu kwa wanawake.

Kama ilivyodokezwa awali, udhalilishaji na kuwapo vikwazo kwa wanawake wakati wa uchaguzi unakwaza utekelezaji wa Lengo Na. 5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) linalozitaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhakikisha zinatilia mkazo usawa wa kijinsia.

Vitendo hivyo pia vinakinzana na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia Tanzania ya Mwaka 2000 inayolenga kuweka mazingira wezeshi, kutatua vikwazo dhidi ya wanawake na kuleta haki na usawa ili kundi hilo lishiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika programu na miradi ya maendeleo.

Hivyo, kuna haja serikali na wadau wa uchaguzi kuondosha vikwazo kwa maslahi ya kundi hilo na ustawi wa jamii ambao ndio lengu kuu la serikali kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ndiyo matokeo ya kuisifia pombe

**IKIWA** wewe ni mtoto na tena bado ni mwanafunzi kumbuka huruhusiwi kugusa vilevi, hata kama utaimbiwa bia tamu. Jiepushe nayo.

Lakini angalia, kwa msisitizo hata vifungashio vya vilevi na viongeza nguvu (energy booster), vimeweka onyo 'hairuhusiwi kutumika na mwenye miaka 18'. Sembuse wewe mtoto wa miaka 12?

Hivyo kwa ujumla watoto na wengine ambao hawajajitambua tena hawajiwezi kimaisha ni marufuku kujihusisha na unywaji wa pombe.

Wakati kukiwa na maelekezo hayo, inaelezwa kuwa baadhi ya watoto wakiwamo wanafunzi, wanakunywa pombe, kitendo ambacho si sahihi kwa maendeleo na ustawi wao kiafya, kisaikolojia na kielimu.

Kutokana na mazingira hayo, mkoa wa Kilimanjaro, umeruhusu kuanzishwa kampeni shuleni kuhamasisha vita dhidi ya ulevi wa pombe unaofanywa na baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari.

Kuanzishwa kampeni hiyo, kunaelezwa na mkuu wa mkoa huo Nurdin Babu kuwa kunatokana na utafiti uliofanywa mwaka 2019 katika mikoa ya Mwanza na Kilimanjaro na kubaini matumizi ya pombe kwa wanafunzi wa shule za sekondari wenye umri wa miaka 15 na zaidi.

Bila kuwataja waliofanya utafiti, anasema, ulionyesha kuwa kiwango hicho cha matumizi ya pombe kwa wasichana kilikuwa ni asilimia 12.9 mkoani Mwanza na asilimia 63.9 kwa wavulana mkoani Kilimanjaro.

Pombe za kienyeji zinazonywewa Kilimanjaro ni pamoja na ndegelua inayotokana na miwa na mbege inayotengenzwa kwa kimea cha ulezi au mbeke.

Wakati Mwanza pombe mashuhuri za kienyeji ni komoni na gongo.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa mkoa, Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika ambako vijana wengi huanza matumizi ya pombe mapema katika umri mdogo, wakiwamo wa kuanzia miaka 15.

Babu alikuwa akizindua kampeni ya kuhamasisha vita dhidi ya matumizi ya pombe kwa wanafunzi shuleni, na kwamba kupitia kampeni hiyo iliyopewa jina la SMASHED inayoendeshwa na kampuni moja ya bia.

Kampeni hiyo ingesambaa nchi nzima ili kunusuru wanafunzi waweze kutimiza ndoto walizojiwekea katika elimu, kwani kunywa pombe kuna athari hasi kwa wanafunzi.

Mojawapo athari hizo ni wanafunzi kujikuta wakiweka mbele kunywa pombe na kuacha masomo, mwisho wake ni kushindwa kutimiza ndoto zao walizojiwekea katika taaluma na maisha.

Kwa kawaida ulevi hauanzi mara moja, bali mnywaji anaanza taratibu na mwishowe anajikuta anakuwa mlevi wa kupindukia.

Hivyo, ni vyema wanafunzi waondolewe katika janga hilo mapema, kampeni hiyo ikisambaa italinda vijana na kuwaepusha na unywaji ambao kama hawatauacha, wanaweza kuwa waraibu badala ya kujitegemea, kumudu maisha yao na kuwa msaada kwa familia zao.

Wataalamu wa afya walishaweka wazi kuwa miili ya watoto na vijana huendelea kukua na kwamba kunywa pombe katika umri mdogo kunaweza kuingiliana na ukuaji wa kawaida wa ubongo na viungo.

Vilevile, wanaeleza kuwa inaweza pia kuathiri viungo muhimu na kusababisha matatizo ya kiafya baadaye maishani, hivyo, kutumia pombe kunaiweka miili yao katika hatari.

Aidha, wanaeleza kuwa kunywa katika umri mdogo, hasa kunywa na kulewa kupita kiasi, kunaweza kusababisha shida za kisaikolojia na kunaweza kuongeza tabia mbaya ya uraibu wa pombe baadaye maishani.

Lakini pia umefika wakati sasa kuzuia matangazo yanayohamasisha unywaji wa pombe au nyimbo zinazohamasisha unywaji kwani inawezekana baadhi ya wanafunzi wamejikita katika unywaji wa pombe kutokana na hamasa hiyo.

Nyimbo na matangazo ya ulevi na uvutaji sigara huwasisimua vijana na kuwaweka katika mazingira ya kupenda kutumia vileo hivyo, ni vyema yakakomeshwa ili kuokoa taifa.

Kwa mfano, kuna tangazo linaloonyesha bia huku kukiwa na maandishi yasomekayo 'fahari yetu', na pia kuna wimbo wa msaani unaosema; 'asikwambie mtu bia tamu'.

Ni kupitia hamasa hizo, pengine baadhi ya watoto wakiwamo wanafunzi, wamejikuta wakijiingiza katika unywaji wa pombe, ambao kama wasipozuiwa, wanaweza kuwa walevi wakubwa wa baadaye.

# FAO yaipa mamilioni taasisi utafiti viini lishe vya vyakula

**Na Renatha Msungu,** ARUSHA

TAASISI ya Kimataifa ya Utafiti wa Kilimo cha Mboga ya World Vegetable Centre, imetia saini mkataba wa mwaka mmoja na Shirika la Chakula Duniani (FAO) wenye thamani ya Dola za Marekani 650,000 (Sh. bilioni 1.652) unaoangalia masuala ya viini lishe na vinasaba kwenye vyakula.

Malengo ya kutia saini mkataba huo ni pamoja na kuongeza uzalishaji mbegu bora katika kituo hicho ambazo zitasaidia wakulima kupata mazao mengi zaidi.

Jana jijini hapa, Mkurugenzi Mkuu Mwandamizi wa

Afrika na Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Word Vegetable Centre, Dk. Gabliel Rugalema, aliwaambia waandishi wa habari kuwa hivi sasa kituo hicho kimekuwa kikubwa.

Alisema kuwa hiyo ndio sababu kwao kuingia mikataba ya kimataifa dunia kwa ajili ya kukiendeleza.

Alisema hivi sasa wana mbegu aina 7,000, lakini hadi kufikia mwakani watafikisha aina 15,000 za mbegu.

"Tumejipanga kuhakikisha tunafikisha idadi hiyo ya uzalishaji mbegu ifikapo mwaka 2025, mbegu zote hizi zitatumiwa na wakulima kwenye kilimo cha mboga," alisema Dk. Rugalema.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha kilimo kinapanuka na kuinua uchumi wa Watanzania hususani vijana wanaojikita zaidi katika kilimo biashara.

Alifafanua zaidi ya kuwa wameamua kuungana na FAO kwa kuwa wote wana nia moja ya kuhakikisha chakula kinakuwa salama kwa Watanzania na duniani kote.

Mbali na hilo, alisema wamekuwa wanapokea wageni wanaofika kujifunza masuala ya kilimo cha mboga, wakichangia kuongeza uchumi nchini.

Dk. Rugalema ameomba Watanzania kutumia mbegu bora kutoka katika kituo chao hicho, akitamba wananchi watarajie "makubwa" kutoka katika kituo hicho baada ya kupata fedha hizo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji mbegu.

Dk. Sognigbe Danikou kutoka FAO alisema wameingia mkataba na kituo hicho ili kukabiliana na baa la njaa barani Afrika.

Aliipongeza taasisi hiyo kutokana na kazi nzuri inazofanya, akiahidi wataendelea kushirikiana nayo kikazi.

Alisema serikali inatoa ushirikiano mkubwa katika kuhakikisha masuala ya chakula kwa jamii yanakuwa sawa, ndio maana nao wameingia mikataba mbalimbali katika ufanyaji kazi za kilimo kwenye taasisi mbalimbali nchini.




Ofisa Uhusiano wa Umma wa Barrick Bulyanhulu, Mary Lupamba, akishiriki upandaji miti katika hafla ya makabidhiano ya miche ya miti kwenye Shule ya Msingi Bulyanhulu kwa kushirikiana na kampuni ya Kakola Digital Solution shuleni hapo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Daraja lililokarabatiwa kwa mil. 42/- lasombwa na maji

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

DARAJA la Mto Msambizi linalotenganisha vijiji vya Lusungo na Songwe, Kata ya Nanyala, wilayani Mbozi ambalo miaka miwili iliyopita lilikarabatiwa kwa Sh. milioni 42, limesombwa na maji na kusababisha kukosekana mawasiliano kati ya vijiji hivyo.

Hali hiyo imesababisha wakazi 20,000 wa Kijiji cha Lusungo kukosa huduma mbalimbali za kijamii, huku wanafunzi 100 wa shule za sekondari wanaotoka katika kijiji hicho wakilazimika kukatisha masomo kwa muda kutokana na kutokuwapo njia mbadala ya kuwafikisha shuleni katika Kijiji cha Songwe.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wananchi hao walisema daraja hilo lilisombwa na maji wiki moja iliyopita baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha usumbufu mkubwa, huku wakiomba serikali kuwajengea daraja la dharura ili kurejesha mawasiliano.

Baadhi ya wananchi, wakiwamo Faines Mbembela na Mpoki Kibona, wote wakazi wa Kijiji cha Lusungo, walisema kukatika mawasiliano ya kijijini kwao na makao makuu ya kata ambako huduma za msingi zinapatikana ni pigo kubwa kwao.

Aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kurejesha mawasiliano hayo kwa dharura ili kuwaokoa na adha wanazozipata, ikiwamo hofu ya wajawazito kukosa huduma muhimu pindi wanapotaka kujifungua.

Diwani wa Nanyala, George Msyani ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, alisema tayari uongozi wa kata umekutana na kufanya tathmini kwa ajili ya kujua kiasi cha fedha kinachohitajika ili kurejesha huduma za mawasiliano ya usafiri katika daraja hilo.

"Tunapata hofu katika siku hizi ambazo serikali inafanya jitihada za kurejesha miundombinu kwa muda ili kunusuru wanafunzi ambao kwa sasa hawaendi shuleni pamoja na watumishi wengine ambao hawataweza kufika katika maeneo yao ya kazi," alisema Msyani.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA), Robert Mwakitalima, alisema wameshafanya tathmini ya gharama za kujenga daraja la dharura na ndani ya wiki moja mawasiliano ya barabara yatarejea.

Mwakitalima alisema TARURA imeomba Sh. milioni 200 kwa ajili ya kujenga daraja la kudumu katika mto huo, ikiwa ni mkakati wa kupata suluhisho la kudumu.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



# HABARI PICHA




Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo (wa pili kulia mwenye miwani), akikabidhi msaada pamoja Taasisi ya 'Sisi na Mama Samia' kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kwenye kituo cha kulelea watoto yatima cha Halima Selengia Orphanage Centre kilichoko Kata ya Bomambuzi mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**



Baadhi ya washiriki wakimsikiliza Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki (hayupo pichani), akizungumza katika Maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani yaliyofanyika kitaifa viwanja vya stendi ya zamani, wilayani Babati, mkoani Manyara mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki (kushoto), akifurahia jambo na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani anayehusika na masuala ya Afrika, Katja Keul (kulia), baada ya kikao kuhusu namna bora ya kushirikiana kwenye kukuza utalii na kuendeleza uhifadhi jana jijini Dar es Salaam.



Dereva akisafirisha shehena ya mzigo iliyojaa kwenye Toyo eneo la Kifuru jijini Dar es Salaam jana na kufanya hasiweze kuona nyuma, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**



Waliokuwa askari polisi wakiwa wameficha sura zao baada ya kutoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana baada ya kesi yao kuahirishwa kutokana na upelelezi kutokukamilika. Watuhumiwa hao wanakabiliwa na mashtaka ya kumteka raia na kumtishia kwa bunduki kisha kumwibia Sh. milioni 90. **PICHA: IMANI NATHANIE**



## KKKT, USAID washirikiana kuinua wanawake, vijana

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), limeahidi kuwasaidia wanawake na vijana wanaotoka kwenye mazingira magumu na hatarishi kupata huduma za afya, elimu na kujenga uchumi wa kaya.

Mkurugenzi wa Wanawake na Watoto wa Idara ya Wanawake ya KKKT, Faustina Nillan, alisema licha ya kuwapatia elimu walengwa wachache waliopata fursa hiyo, kanisa hilo kwa kushirikiana na USAID, wameanza kuwainua vijana kujikwamua kiuchumi na kuwajengea uwezo wa usimamizi wa fedha.

Akizungumza jijini hapa wakati wa makabidhiano ya mashine za kushonea nguo zenye thamani ya Sh. milioni 11, alisema kundi la vijana, limenufaika na miradi inayoendeshwa na idara hiyo, baada ya kufadhiliwa kupata ujuzi katika Chuo cha Ufundi Stadi Nchini (VETA), ili kuwasaidia kujikwamua na wimbi la umaskini.

"Wanufaika hawa kwa sasa, wanaweza kusimamia fedha wanazozipata, lakini wameweza kujikwamua kiuchumi. Kama alikuwa anatumia shuka lililotoboka, leo anajifunika shuka nzuri.

"Kama walikuwa wanatumia kikombe cha plastiki, kwa sasa wanaweza kununua seti ya vikombe vya udongo, na hata vibaka wamepungua kupitia mradi huu."

Akitoa taarifa kuhusiana na Mradi wa USAID, Msimamizi wa Mradi huo, Vaileth Mollel, alisema mradi huo unatekelezwa katika mikoa tisa na kati ya mikoa hiyo, mikoa mitatu pekee inasimamiwa na KKKT.

"Mikoa mingine inayobaki inasapotiwa na USAID, ambapo kwa mwaka huu tunatarajia kufikia walengwa 157,110 kwa maana ya wanawake na watoto wanaotoka katika mazingira magumu na hatarishi, wakiwapatia huduma za afya, elimu na kujenga uchumi kwa kaya husika.

# Mwarobaini kudhibiti wanyama pori kuharibu mali wapatikana

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SERIKALI imepata mwarobaini wa wanyamapori wakali na waharibifu wanaovamia makazi ya watu, baada ya kuanzisha mfumo wa kidijitali wa kuwabaini wanyamapori wanaotoka hifadhini na kwenda kwenye makazi ya watu.

Kwa mujibu wa Ofisa Wanyamapori wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Nassoro Wawa, mfumo huo wa kisasa utaonyesha bayana mnyama anapotoka hifadhini na uelekeo wake anapokwenda.

Mtaalamu huyo aliyasema hayo jana wilayani Babati, mkoani Manyara wakati wa kilele cha Siku ya Wanyamapori Duniani.

"Kama anaonekana kwenda kwenye makazi ya watu, itakuwa rahisi kuchukua hatua mapema za kumrudisha, ili asiende kuleta madhara katika mashamba na makazi ya wananchi," alisema.

Kuanzia sasa, wanyamapori wote hasa tembo watavisha kola zijulikanazo kama visukuma mawimbi kwa ajili ya kutambua mwelekeo wao kwa ajili ya kuwazuia kuingia katika makazi ya watu.

Alisisitiza kuwa kupitia njia hiyo, askari wa uhifadhi watakuwa na uwezo wa kuwafuatilia kwa karibu, na endapo kundi lolote la tembo litakuwa na mwelekeo wa kuingia kwenye makazi ya watu, watalizuia kabla ya madhara kutokea.

"Makundi ya tembo ambayo yanaonekana kuzagaa tutayaingiza kwenye mtambo na tembo viongozi tutawafunga kola zijulikanazo kama visukuma mawimbi na tutawafuatilia wameenda wapi," ameeleza ofisa huyo wa wizara.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Regina Ndege (katikati), akimbeba mtoto baada ya kugawa mashuka 50 kwenye hospitali ya rufani ya mkoa huo na misaada mbalimbali kwa wagonjwa wa hospitali hiyo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Namna kilimo ikolojia kitakavyobadilisha maisha

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

WAKULIMA wa Wilaya za Arumeru, Monduli na Longido, mkoani Arusha, wameanza kutumia dhana ya kilimo ikolojia, kuzalisha wadudu wenye tija wakiwamo vipepeo na nyuki kwa ajili ya kuboresha uchumi wa jamii.

Kilimo ikolojia wilayani humo, kinatumika hivi sasa kwa ajili ya kupunguza matumizi makubwa ya upuliziaji wa kemikali za sumu kwenye mimea, inayotumika kwa uzalishaji wa chakula.

Kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima wa wilaya hizo wanaojishughulisha na kilimo ikolojia, wameitaka serikali na wadau wa sekta hiyo nchini, kuendelea kuhamasisha juu ya matumizi ya kilimo ikolojia (kilimo hai) na kutenga bajeti ya kilimo hicho chenye tija katika ushindani wa soko la kimataifa.

Wakizungumza katika jukwaa maalum la wadau wa kilimo ikolojia lililoandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Island of Peace, ambalo limejitosa kuwajengea uwezo wakulima na wafugaji kuhusu urejeshaji wa baionuai, mbinu za utunzaji wa mazingira na matumizi ya mbegu za asili, walisema mbinu hiyo mpya itasaidia kuboresha maisha yao.

Antony Mbise, Mkazi wa Oldonyowasi, Halmashauri ya Arusha, alisema kwa kuwa kilimo ikolojia, kina mfumo jumuishi wa uzalishaji unaotegemeana, unaopunguza uharibifu wa mazingira, na kuwa na mwingiliano wa kirafiki wa viumbe hai vilivyoko ardhini, ni vyema Wizara ya Kilimo ikafikiria zaidi kukiinua kilimo hicho.

Mmoja wapo wa wawezeshaji wa kilimo ikolojia, Erwin Kinsey, ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la ECHO, alisema iko haja ya kutumika kwa mbinu za asili za kutunza mazao, ili kuzuia wadudu waharibifu, unyevu katika mazao pamoja na wizi.

"Zipo njia nyingi za asili za kutunza mazao yasiharibike, lakini mojawapo ni ya kuchimba shimo ndani ya nyumba, kuweka plastiki, mchanga na kufukia.

"Kwa hiyo mbinu, wadudu hawawezi kupenya, lakini hakuna unyevu na ni ngumu sana mwizi kuweza kuiba. Vilevile inatumia gharama kidogo sana na ina kinga wadudu waharibifu," alisema Kinsey.

Aidha, Erimelinda Temba kutoka Shirika la Island of Peace, alisema wakulima wengi hawana uwezo wa kumudu gharama za kununua dawa na mbolea, kwa ajili ya kustawisha mashamba na kuua wadudu na magonjwa kwenye mazao yao, hivyo kilimo ikolojia, kinaweza kuwa msaada mkubwa kwa wakulima na jamii za klifugaji.

"Kilimo ikolojia ni mbinu shirikishi iliyounganishwa, ambayo inatumika kwa wakati mmoja kwa kutumia dhana, kanuni za ikolojia na usimamizi wa mifumo endelevu ya kilimo na chakula.

"Mfumo huo unalenga kuboresha mwingiliano kati ya mimea, wanyama, binadamu na mazingira. Kilimo ikolojia kinashughulikia hitaji la mifumo ya chakula yenye usawa wa kijamii, ambayo watu wanaweza kufanya uchaguzi juu ya kile wanachokula, jinsi na wapi kinazalishwa.

Kilimo ikolojia ni muhimu katika kupunguza mnyororo wa mazingira ya kilimo, kuhakikisha mazingira endelevu, yenye afya ili kuhakikisha kunakuwapo na usalama wa chakula na lishe."

Alisema washiriki wa jukwaa hilo ni wadau wa kilimo, wafugaji, wakulima, washiriki kutoka vyuo vya elimu, taasisi za serikali wakiwamo maofisa ughani na wanaharakati.





# Rais akabidhi mashine ya kuchapa kwa watoto

**Na Benny Kingson,** TABORA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameikabidhi Taasisi ya Mafanikio Foundation inayojihusisha na malezi na makuzi kwa watoto mkoani Tabora msaada wa mashine ya kuchapa ikiwa ni sehemu ya kutimiza ombi lao katika kurahisisha ufundishaji.

Akikabidhi mashine hiyo juzi kwa niaba ya Rais, Mbunge wa Viti Maalum CCM Mkoa wa Tabora, Aziza Sleyum alisema Rais Samia ametoa msaada huo kufutia adha walizokuwa wakikabiliana nazo hasa wakati wa kuchapa mitihani ya watoto katika vituo vyake.

"Rais Samia ameniagiza niwakabidhi mashine hii ambayo itawasaidia katika shughuli zenu kuandaa mitaala ya kiserikali na hata ya kidini ili watoto hawa ambao ni wajukuu wake wapate huduma katika kituo chenu," alisema Sleyum.

Aidha, aliwataka wazazi, walezi, walimu pamoja na jamii kwa ujumla kuwafuatilia watoto na kusisitiza kuzishika imani zao na maadili mema wakati wote na popote na kuwasimamia katika kila jambo na kuwawekea mazingira bora na yenye usalama.

Kuhusu gharama za mashine hiyo, Sleyum alisema Rais Samia hakutaka zitajwe na kuwa lengo lake ni kuhakikisha watoto wanapata mahitaji yao staki ya kielimu na kutimiza ndoto zao.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Mwalimu Amiri Mikombe alisema wana vituo 30 vya malezi na kufundisha pia ina



watoto 930 na kwamba wanahudumia katika Wilaya za Tabora Mjini, Nzega, Sikonge, Urambo na eneo la Usoke wilayani humo.

Mwalimu Mikombe alisema kuwa awali walipata shida sana kuandaa mitihani ya watoto na nyaraka mbalimbali za kuwafundishia ambapo huduma hiyo waliipata kwa gharama kubwa na wao hawakuwa na uwezo na ndipo walipoamua kumwomba Rais mashine hiyo waliyopokea.

"Kwa sasa tumebaki na uhaba wa viti vya kukalia ambapo tuliwaomba watu wahudhuria hafla hii ili kusaidia kuchangia tupate viti 1,000 ambapo tumefanikiwa kupata mchango wa fedha taslimu Sh. 84,400, ahadi Sh.100,000 na ahadi ya viti 212 na wengine waliahidi kuendelea kuunga mkono changizo hili," alisema Mikombe.

Shekh Mahafudhi Anam aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha watoto wanapelekwa katika mafunzo ya dini kulingana na imani zao na kuacha mtindo wa kuwaita walimu majumbani kuwafundisha, kwa kuwa elimu hiyo siyo sahihi kama ile ya darasani.



Mratibu wa Mradi wa Tuwaandae Pamoja kutoka Shirika la Tanania Early Childhood Education and Care (TECEC), Ester Macha ambaye ni mtaalamu wa kuandaa zana za watoto za kujifunzia utambuzi, akitoa elimu ya malezi ya awali kwa wazazi na walezi jijini Mwanza juzi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# 100 wanusurika kifo mabasi yakiviziana kupita

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MABASI mawili yaliyokuwa safarini kuelekea mjini Kahama kutokea mkoani Kagera na Arusha yamegongana katika njia ya mzunguko, Mtaa wa Phantom Manispaa ya Kahama wakati yote yakilazimisha kupitia katika mzunguko huo kwa wakati mmoja ili kuingia kituo kikuu cha mabasi mjini hapa.

Katika ajali hiyo iliyohusisha basi kutoka kampuni ya Marangu Coach lenye namba za usajili T 452 DKG na Mumuk Investment lenye namba za usajili T 291 ATH ilitokea juzi majira ya jioni ambapo abiria wote 100 walinusurika huku madereva wote wakitokomea kusikojulikana.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, alisema hakuna kifo chochote wala majeruhi isipokuwa baada ya kutokea kwa tukio hilo madereva wa magari hayo walikimbia kusikojulikana na kuwataka kujisalimisha kabla hatua za kuwatafuta hazijaanza.

Alisema kwa sasa wanaendelea na utaratibu wa kuyaondoa magari hayo ambapo moja lilitumbukia mtaroni na kuruhusu shughuli nyingine kuendelea.

Mmoja wa shuhuda wa ajali hiyo, Hamisi Juma alisema uzembe wa madereva wa mabasi hayo ulichangia kutokea kwa ajali hiyo kwa kuwa walikuwa wakifukuzana kwa mwendo kasi, ili kupita barabara hiyo ya mzunguko ilihali walikuwa tayari wamefika.

Mmoja wa abiria aliyekuwa katika basi la Marangu Coach, Matha Samwel alisema dereva wa basi hilo alikuwa mwendokasi tangu wanatoka Arusha walikuwa wakishindana na mwenzake, lakini walipopaza sauti hakutaka kuwasikiliza hadi walipofika Kahama gari lao lilipopata ajali.

Aidha, wameiomba serikali kuwachukulia hatua kali madereva hao ili kuepusha matukio yanayogharimu maisha ya watu na miundombinu.

# Shirika laonya malezi kisasa yanayoharibu watoto

**Na Zatifa Ramadhan,** SAUT

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Tanzania Early Childhood Education (TECEC) limeitaadharisha jamii hususani wazazi juu ya mwenendo unaotajwa kuwa wa kisasa katika malezi ya watoto unaohatarisha maisha yao ya baadaye.

Mienendo hiyo inajumuisha matumizi ya muda mrefu ya simu kwa watoto, televisheni, miziki ya kisasa pamoja na watoto kutokupata nafasi ya kucheza michezo ya matumizi ya viungo vyote vya mwili, ili kuchangamsha akili na viungo hivyo.

Tahadhari hiyo imetolewa juzi na Mkurugenzi wa TECEC, Joel Elphas wakati wa kutambulisha Mradi wa Tuwaandae Pamoja kwa wazazi wa Kata ya Luchelele wilayani Nyamagana mkoani Mwanza, sambamba na semina ya malezi, makuzi ya watoto na utambuzi wa elimu ya afya kwa watoto wenye umri kuanzia miaka sifuri mpaka minane.


Alisisitiza umuhimu wa matumizi ya lugha thabiti kwa watoto tangu wakiwa tumboni, ili kuwawezesha kufikia ukuaji na maendeleo yao kamili akitaja hatua hiyo kuwa na athari kubwa kwa maisha ya baadaye ya mtoto huyo.

"Kwa mtoto wa sifuri mpaka miaka miwili hatakiwi kabisa kutumia simu wala kutazama televisheni na pia wale wa miaka miwili kwenda juu alitazama televisheni na simu awe na mtu wa kumsimamia kwa vipo vitu vingi vya ajabu vinavyoweza kuathiri moja kwa moja mfumo wa ubongo wa mtoto," alisema Elphas.

Mtaalamu wa utengenezaji wa zana za kujifunzia kwa watoto na mratibu wa mradi huo alitoa mbinu na njia za jinsi wazazi wanavyoweza kusaidia katika kukuza uwezo wa watoto wao kupitia michezo na shughuli za kielimu na kusisitiza umuhimu wa kutoa mazingira mazuri ya kujifunzia nyumbani ili kusaidia ukuaji wa ubongo wa mtoto.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 5, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 12


Ukurasa 13
Mwinyi ndiye alifunua siri ya kufanyika biashara Tanzania


Ukurasa 14
**AMINA SALUM: Mwinyi ni chanzo cha mafanikio yangu kisiasa**

ELIMU
**NA MWANDISHI WETU**

## KUMBUKIZI ZA MWINYI 1925 -2024

# Ni kiongozi aliyekubalika kila kona, 1990 Papa Yohane Paulo alimtembelea

### •Alikuwa Rais aliyejishusha, akiishi kama mtu wa kawaida mno


Mzee Ali Hassan Mwinyi (kushoto) na mgeni wake Papa Yohane Paulo wa II. **PICHA: MTANDAO**

NI siku kwaya zilipoimba kwa furaha... Baba Mtakatifu wetu amekuja kututembelea. Septemba tarehe mosi ni shangwe hapa Tanzania...” Ndivyo Dk. Peter Kafumu, anavyokumbuka wimbo ulioakisi ujio wa Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Yohane Paulo wa II.

Alizuru Tanzania Septemba 1,1990 alipotua Dar es Salaam alikaribishwa na Rais wa Tanzania, Ali Hassan Mwinyi, hivyo Papa alikuwa mgeni wa Rais Mwinyi.

Kafumu anaeleza kuwa ulikuwa ugeni mkubwa wa Yohane Paulo II, kukanyaga ardhi ya Tanzania katika Uwanja wa Julius Nyerere na kubusu ardhi yake. Kwa siku tano alitembelea Dar e Salaam, Songea, Mwanza, Tabora na Moshi zikizizima kwa ujio wa kiongozi huyo, aliyelenga kuimarisha imani ya Wakatoliki na ushirikiano kimataifa.

Dk. Kafumu aliyewahi kuwa Mbunge wa Igunga (CCM), anasema chini ya uongozi, hekima usimamizi na uthabiti wa Rais Mwinyi, Papa John Paul II, aliingia na kutoka Tanzania akiwa salama.

“Kuamua kuja Tanzania ni heshima kwa taifa ambayo inamgusa mkuu wa nchi -Rais Mwinyi,” anasema Kafumu, aidha alizuru Burundi, Rwanda na Cote d’Ivoire au Ivory Coast.

Akizungumzia ziara hiyo, Dk. Kafumu, anasema aliishuhudia na kwamba Mwinyi, alionyesha kuwa serikali yake haikuwa na dini lakini raia ndiyo wenye dini mbalimbali na inashirikiana na wote kuleta ustawi wa taifa.

Anamsifu zaidi, Mzee Mwinyi, akisema kwa ujumla alikuwa Rais na kiongozi mkuu wa taifa na serikali ambaye aliamua kujishusha, akaishi kama mtu wa kawaida sana, mnyenyekevu, kama wengine lakini si kwa kulazimishwa bali kwa kuamua mwenyewe.

“Kule kuwa rais hakuona ni kitu cha kujivunia, kutanua misuli na kutaka aonekane mkubwa na mashuhuri bali alijishusha na kuwa mtu aliyeishi maisha ya kawaida tofauti na madaraka na cheo alichokuwa nacho.” Anasema Dk. Kafumu aliyewahi kuwa Kamishna wa Madini, wakati wa awamu ya nne.

### HAKUWASAHAU WATU

Mwinyi ni mpenda nasaba (ndugu) aliyewaendeleza udugu na kuwafuatilia watu wengi alioshirikiana nao kuanzia viongozi na marafiki ambao amekuwa nao kwenye majukumu mbalimbali ya kijamii na kiuongozi.

Ni sifa anayopewa na mkuu wa wilaya mbalimbali mstaafu, Athuman Mdoe, ambaye licha ya wote kuondoka kwenye uongozi Mzee Mwinyi, hakumsahau na muda wote waliendelea kuwasiliana na kuendeleza umoja na udugu.

Mdoe aliyekuwa Mkuu wa Wilaya za Ilala na Kinondoni jijini Dar es Salaam, anasema Mwinyi alikuwa anampokea, kumsikiliza na kumsaidia yeyote aliyehitaji msaada kwake.

Aidha, anasema kwa upande wa viongozi aliofanya nao kazi hakuwasahau na kila wakati aliwatafuta kuendeleza ushirikiano wa kidugu na kirafiki licha ya kwamba alikuwa ameondoka serikalini.

### TANZANIA YA WALIMU

Mwinyi aliyeondoka Ikulu Novemba 1995, ameendelea kuacha historia kuwa Tanzania ni taifa lililoongozwa na walimu, akianza Mwalimu Julius Nyerere, akifuatiwa na Mwalimu Mwinyi.

Kama Nyerere alivyosomea alianza kusoma Makerere Uganda kisha Edinburgh Scotland na kuanza kufundisha Pugu Sekondari, Mzee Mwinyi alisoma Chuo Kikuu cha Hull Uingereza, baada ya kurejea akafundisha shule za Msingi Mangapwani ambayo sasa ni sekondari na kisha kuhamishiwa Bumbwini ambayo pamoja na kuifundisha ni mwanzilishi akitumia nguvu na fedha zake kuijenga.

Wakati alipoichukua nchi mwaka 1985, wachache walitarajia mwanasiasa huyo mpole, mwenye aibu na asiyejivuna, aliyefariki Alhamisi wiki iliyopita ‘angeishepu’ Tanzania kwa kufanya mambo yanayoonekana leo. Kwa kifupi ndiye aliyeyaasisi.

Amefariki dunia akiwa na

INAENDELEA UK.12

# Ni kiongozi aliyekubalika kila kona, 1990 Papa Yohane Paulo alimtembelea

INATOKA UK.11

miaka 98, lakini ameacha alama ya kuibuka kiongozi mwenye kuleta mabadiliko, mageuzi ya kiuchumi, kisiasa, fikra, mitizamo na hata mienendo ya watu kuanzia wakati huo hadi sasa.

Mwinyi anaugeuza uchumi uliokuwa umedorora na kuanzisha mfumo wa kiliberali na demokrasia ya vyama vingi katika taifa hili ambalo wengi walikuwa waoga hata kuuza pipi mitaani kutoka na fikra za kijamaa walizokuwa wamekulia.

Mzee Mwinyi aliaminiwa na shujaa wa Uhuru Mwalimu Nyerere, akikubali arithi nafasi yake na kuiongoza nchi kuivusha kwenye misukosuko ya kiuchumi, baada ya miongo miwili ya siasa za ujamaa kushindwa.

Ujamaa na Kujitegemea iliyokuwa sera kipenzi cha Nyerere iliyokuwa unalenga kuwaleta pamoja Watanzania wote na kukuza uchumi unaomilikuwa na dola, uliposhindwa uliliacha taifa kwenye mkwamo na hali mbaya ya uchumi iliyohitaji tabibu, ndiye Ali Hassan Mwinyi.

Mwinyi aliingia chumba cha upasuaji na kuufumua mfumo wa uchumi akiondoa vikwazo kwa wawekezaji binafsi na kupunguza vikwazo vya kuagiza bidhaa nje badala ya kutegemea viwanda vya ndani ambavyo vilikuwa taabani na kuamua kuwa sasa ni ruksa kwa soko na uchumi huria.

Mzee Rukhsa, hakusita kuchukua hatua akija na maazimio kadhaa likiwamo la kuachana na Ujamaa na Kujitegemea kwenye itikadi ya uchumi na kueleza kuwa siasa hiyo ilikuwa inanyonga wafanyabiashara wadogo.

Uchumi wa Tanzania ulikuwa ukikabiliwa na changamoto kupindukia ambazo baadaye zilibainika kuwa nyingi zilitokana na muundo wa uchumi, hivyo Mwinyi baada ya kuona hayo, alitangaza nia ya kuurekebisha mfumo huo.

Akizaliwa Mei 8, 1925 katika Kijiji cha Kivure Mkuranga, mkoani Pwani, alihamia Zanzibar kujifunza dini -Uislam, wakati huo familia yake ikimwandaa kuwa kiongozi wa kiroho, lakini kijana Mwinyi alijiendeleza zaidi kidini na kitaaluma akawa mwalimu na kufundisha shule kadhaa kisiwani Unguja , kabla ya kuingia kwenye siasa miaka ya 1960 baada ya Uhuru wa Tanganyika.

Kubwa ni kufungua milango ya demokrasia ya vyama vingi mwaka 1992 na kuruhusu vyama vya upinzani kugombea nafasi za



Mzee Ali Hassan Mwinyi

ubunge, urais, udiwani kwenye uchaguzi miaka mitatu baadaye, alipong'atuka na kumwachia Benjamin Mkapa usukani kuliongoza jahazi la Tanzania.

Mageuzi ya kiuchumi aliyoyaongoza yaliambatana na vikwazo kadhaa mfano biashara za magendo ya bidhaa, hata biashara haramu pamoja na kujenga mifumo mipya baada ya ile ya awali kuporomoka.

Mpaka Mwinyi aliposhika madaraka ya urais wa Tanzania mwaka 1985 ndipo ukweli kuhusu mwelekeo na kasi ya mageuzi ya kiuchumi ilipopamba moto.

Ndiye aliyeidhinisha Mpango wa Kufufua Uchumi mwaka 1986 ukiitwa Economic Recovery Programe (ERP), ambao ulijaribu kufufua pato la taifa, kupunguza nakisi ya biashara na bajeti na kudhibiti mfumuko wa bei.

ERP ilitumika kama msingi wa mazungumzo na Shirika la Fedha la Kimataifa IMF baadaye mwaka huo huo na kisha ujio wa mikopo kutoka Benki ya Dunia (WB).

Baada ya kuamua kijasiri, Tanzania kuchagua kurudi katika mfumo wa vyama vingi ndipo ilipofikia kupatikana hali ya hewa mpya ya kisiasa iliyoimarisha sera za uchumi wa soko huria.

**ALIKOMESHA RUZUKU**

Mwinyi hakufanya ajizi alijua kuwa mashirika ya umma yalikuwa furushi la misumari lisilobebeka. Aliona ni wakati wa kifo cha mashirika hayo na kuondolewa kwa mfumo ambao serikali iliyalinda, tena kuyatunza ikiyaendesha kwa fedha za ruzuku licha ya kwamba yalikuwa hayana tija.

Zaidi ya mashirika 400 yalikuwa hodhi yakiendeshwa kwa ruzuku ya serikali kuanzia NMC au shirika la usagishaji la taifa lililokuwa likinunua mahindi na ngano na nafaka nyingine nchi nzima na kusaga unga.

Jijini Dar es Salaam lilikuwapo shirika la ugawaji na usambazaji NDL lililokuwa likisambaza bidhaa kama unga, mikate, sukari mitaani kwa wateja wa kaya kwenye maeneo yote.

Mashirika ya viatu kama Bora Shoes, NMC, Kampuni za Biashara (RTCs) na kampuni za uchukuzi za mikoa (RATCOs), taasisi zote hizo zilitegemea ruzuku ya serikali na ujio wa Mwinyi uliziondolea ruzuku na huo ukawa mwanzo wa kufa.

Mashirika mengi yalikufa na ilipofika mwaka 1995 karibu yote yalikuwa 'yamezikwa' na bidhaa nyingi zilikuwa zinaagizwa kutoka nje huku mitumba kuanzia mavazi, vyombo vya ndani, vifaa vya kielektroniki kama redio, runinga na friji vikipatikana kwa wingi.

Mwinyi aligundua kuwa mashirika mengi ya umma yalikuwa mzigo na yaliyokuwa na madeni yasiyolipika. Aidha, wachache waliendelea kuyatumua kujinufaisha mfano mameneja na wakurugenzi walijitengenezea utajiri kupitia uhaba mkubwa wa bidhaa na huduma wakishirikiana na walanguzi kuziuza kwa kificho.

Walitengeneza pesa na utajiri kupitia kuuza na kusambaza bidhaa adimu na hilo lilikuwa ni ubia kati ya vigogo hao na wafanyabiashara binafsi ambao waliuza bidhaa adimu kwa kificho na hilo lilihitaji kudhibitiwa kwa kuyafuta au kuyafungilia mbali .

Mrithi wa Mwinyi, Benjamin Mkapa, alitimiza azma hiyo kwa kuyanadi mashirika hayo, akianzisha Taasisi ya Kurekebisha Sekta ya Umma au Presidential Parastatal Sector Reform Commission -PSRC.

**KWA VIJANA LEO**

Ingekuwaje bila Mzee Mwinyi? Hata saloon ukiona leo 'JJ Barbershop' au Queen Beaty Saloon' ni juhudi zake. Atabaki vichwani mwao wengi kwamba ndiye aliyefungua milango ya kuwapo teknolojia nyingi wanazotumia leo kuanza runinga, simu za mkononi, kompyuta, friji za kisasa, viyoyozi na vifaa vingi vya kidijitali ambavyo wakati wa Mwalimu vilionekana kuwa ni anasa tena havikuwapo kwa Watanzania wengi.

Nguo za mitindo ya kileo kama jeans, raba za 'fasheni' mbalimbali, pamoja na vipodozi kwa wanawake kuanzia kupata nywele bandia au wigi au rasta, manukato, sabuni na hata mapambo kama mikufu bangili na hereni viliingia kwa wingi na huo ukawa ndiyo mwanzo wa kuanzisha huduma za saluni za kike na kiume.

Vijana wanaozungumza na Nipashe wanasema ndiye aliyebariki kuwapo na watu wanaojipamba wanaooneka leo.

Kipindi cha Mwalimu Nyerere hakukuwa na magari mengi binafsi. Magari madogo yalikuwa machache, tena mengi yakiingizwa kijanja. Taasisi zilitumika kuingiza magari binafsi kwa kificho.

Serikali ndiyo ilikuwa mmiliki mkuu lakini Mwinyi akaruhusu magari nayo yakimiminika vya kutosha kuanzia mitumba na mapya.

Ukawa mwanzo wa kujenga gereji kila mtaa na kuanzisha maduka ya kuuza magari ambayo hata leo yanaendelea kuongezeka.

Licha ya juhudi za kuufungua uchumi wapo waliotumia milango hiyo kuingiza na kuuza bidhaa haramu ambazo zimewaathiri wengi hasa mijini.

**KULETA UTHUBUTU**

Huyu ndiye mwanzilishi wa uthubutu. Ni baada ya kuruhusu kuingia fikra mpya kwenye biashara, uwekezaji na uthubutu miongoni mwa Watanzania ambao awali haukuwapo.

Kwa mfano alikubali kuanzishwa vyombo vingi vya habari kuanzia mwanzoni mwa 1990 na alishiriki mwenyewe kwa furaha na bashasha kuvizindua pale alipoalikwa.

Uthubutu unakuja pale anapofanikisha kuwapo taasisi nyingi za kiuchumi na kibiashara ambazo zinawapa vijana mwamko na fursa za kujiingiza kwenye kazi ambazo walikuwa hawazifahamu wala kuzisomea lakini wakapata ujasiri wa kuzifanya pamoja kupewa ujuzi kazini wakafanikiwa.

Kwa mfano, licha ya kwamba waandishi wa habari hawakuwa wengi kitaaluma ujio wa vyombo binafsi vya habari uliwaibua mamia ya vijana kwenye ajira hiyo ambayo imeendelea kubadili maisha ya wengi.

NA MWANDISHI WETU

# Mwinyi ndiye alifunua siri ya kufanyika biashara Tanzania



Mzee Ali Hassan Mwinyi kwenye majukwaa ya uongozi. **PICHA: MTANDAO**

BAADA ya Rais Ali Hassan Mwinyi, kuchukua usukani wa kuiongoza Tanzania 1985 alifungua siri ya kuanzisha na kunawiri biashara kwa kila mtu.

Awali biashara ilionekana kama jambo ambalo si jema, pengine 'dhambi' au shughuli ambayo haikuwa na nafasi kubwa katika jamii ya Mtanzania.

Baadhi ya mashuhuda wa namna Mwinyi alivyofunua siri ya kunawiri kibiashara ni Dk.Donath Olomi, Mtendaji wa Shirika la IMED Tz, pia mhadhiri mstaafu wa masuala ya biashara, ujasiriamali na uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Anaeleza kuwa Mwinyi alipoingia kazini, mishahara ya wafanyakazi wa umma ilikuwa haitoshi, akawaambia watumishi kila mtu atumie maarifa yake aweze kuishi.

Anasema katika zama hizo watu walifanyakazi mpaka siku za Jumamosi, lakini akabadilisha utaratibu kuwa kazi zifanyike kwa siku tano za juma na Jumamosi yawe mapumziko ya mwisho wa wiki, ili watu wafanyekazi zao kuendesha maisha yao.

Huo ukawa mwanzo wa ujasiriamali na utafutaji, zikaibuka biashara ndogo kwa kubwa, yakajengwa maduka, kampuni binafsi zikaanzishwa kuanzia ujenzi, ukandarasi, hoteli, nyumba za wageni na maduka ya nyama na ufugaji wa aina mbalimbali, anaeleza Dk. Olomi.

Anakumbusha kuwa Mwinyi aliuona uhaba mkubwa wa bidhaa na kutangaza kuwa yeyote anaweza kuagiza bidhaa popote hatazuiliwa wala kuulizwa amekuwaje na huo ukawa mwanzo mwingine wa kuleta fikra za uthubutu, utafutaji na ujasiriamali.

Mtaalamu huyo wa uchumi, ujasiriamali na masuala ya sekta binafsi, anakiri kuwa Mzee Mwinyi, amewafumbua watu macho wakaanza kuangalia fursa ndani na nje ya mipaka akifungua tena biashara za mipakani zilizokuwa zimezuiliwa baada ya Tanzania kufunga mipaka yake na Uganda na Kenya.

> "Viwanda havikuwa na uwezo wa kuzalisha bidhaa muhimu zinazotosheleza mahitaji, hata zilizozalishwa zilikuwa mbovu, kulikuwa na madeni ya nje na ndani, pia uzembe kwenye utendaji kazi serikalini na kila kitu kilidorora." Anasema.

Aidha, anakumbusha kuwa Mwinyi alipoingia madarakani alikuta nchi ikiwa taabani na akalazimika kufanya juhudi za ziada ili taifa liendelee na kwamba wakati huo nchi haikuwa na akiba ya dola au fedha za kigeni, iliumizwa na uhaba mkubwa wa bidhaa muhimu.

"Viwanda havikuwa na uwezo wa kuzalisha bidhaa muhimu zinazotosheleza mahitaji, hata zilizozalishwa zilikuwa mbovu, kulikuwa na madeni ya nje na ndani, pia uzembe kwenye utendaji kazi serikalini na kila kitu kilidorora." Anasema.

Anaeleza kuwa Mzee Mwinyi alilazimika kufungua na kubadili hali ya nchi, mageuzi ambayo pia aliyasimamia kikamilifu, ikizingatiwa kuwa hakukuwa na mbadala kuliko vile alivyofanya.

Inavyoelekea hatua nchi iliyofikia hata Mwalimu Nyerere, angelazimika kubadilisha mwelekeo kama Mwinyi, anasema Dk. Olomi.

Halikadhalika, anasema Mwinyi ndiye aliyeifungua nchi na kubadili mwelekeo uliokuwapo akifanya mambo ambayo watu waliokuwapo serikalini kwa muda mrefu wasingeyaweza.

Kwa muda mfupi aliokuwapo serikalini, hakuwa sehemu ya Kamati Kuu (NEC) ambayo ilikuwa ikifanya maamuzi mengi makubwa au mazito, lakini kiongozi huyo aliamua na kusimamia yale aliyoyaamini akionyesha ukomavu na utofauti kuliko waliokuwa karibu na Mwalimu Nyerere.

Anakiri kuwa upeo aliokuwa nao ni tofauti na ule wa viongozi au wanasiasa waliokuwa wakiendesha serikali.

"Kazi zake zilitoka hata nje ya mipaka na leo kila mmoja anazishuhudia hasa kwenye uchumi na utafutaji ambao unawagusa karibu watu wa rika na jinsia zote." Anaongeza mchumi huyo.

Mwinyi alifungulia mabadiliko kwenye biashara za mipakani kwenye nchi za Afrika Mashariki baada ya kushika uongozi wa Tanzania, lakini ikifuatiwa na kuondolewa utawala wa Idd Amini Uganda.

Mabadiliko hayo yalianzisha ruksa mipakani na uhusiano mwingine kwenye biashara Afrika Mashariki, anasema.

Mabadiliko ya uchumi kwa Tanzania aliyoyaleta Mwinyi yaliongeza ukuaji wa biashara ndani ya Afrika Mashariki hata leo mfano uwekezaji wa kampuni za wazawa.

Mwinyi aliondoa ukiritimba kwenye biashara kwa kuwa bidhaa ziliagizwa nje na serikali pekee na waliotaka waliomba vibali na pia ilidhibiti bei zilizosimamiwa na Tume ya Bei.

### CHANGAMOTO KIBIASHARA

Licha ya nia njema ya kufungua milango, awamu ya ruksa ilisababisha ilikutana pia biashara haramu ambazo zilijipenyeza kwenye nia njema ya kuwa na Tanzania yenye soko huria.

Katika maelezo yake aliwahi kusema kuwa unapofungua madirisha utapata hewa safi lakini wadudu na vumbi pamoja vingine usiyovihitaji vitaingia, ndiyo maana baada ya kufungua madirisha wadudu wabaya kama rushwa, dawa za kulevya, utapeli wa ardhi na uporaji wa mali za umma na za binafsi uliota mizizi.

Hata hivyo sababu kubwa ya vitu hivyo kuzidi ni kwa vile taasisi zilizokuwa zikisimamia uchumi, biashara na mifumo ya kuendesha nchi zilikuwa na sura ya kijamaa na zilikuwa hazijabadilishwa, anakumbusha Dk. Olomi..

Dokta Olomi, akifanyakazi na IMED Tz, shirika lake linaendeleza harakati za kuifungua na kuwajenga Watanzania kwenye biashara za kisasa kwa mfano kufundisha ujasiriamali, utafutaji, kuendeleza na kupanua kisasa zaidi sekta binafsi na biashara.

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

## AMINA SALUM:

# Mwinyi ni chanzo cha mafanikio yangu kisiasa

• Ameibua na kuwalea wanawake, yumo Bi. Kidude

NI mwanamama mwenye ushawishi katika masuala ya uongozi, akianzia kwenye uwaziri, ubalozi na hata kuwania urais Zanzibar na Tanzania.

Leo anafichua chanzo cha mafanikio yake akisema, kila unaposikia jina na historia ya maisha na vipawa vyake vikitajwa, aliyemwibua ni Mzee Ali Hassan Mwinyi.

Ni Balozi Amina Salum Ali, anayesema hayo akizungumza na Nipashe mjini Zanzibar, wakati wa maombolezo ya kifo cha Mzee Mwinyi.

Anasema ni pigo kwake binafsi na taifa kutokana na mambo makubwa aliyofanya kiongozi huyo katika maisha yake, wanawake, wasanii, taifa pote Bara na Visiwani.

Kwake Mzee alikuwa mlezi na ndiye aliyemwinua katika ngazi za uongozi hadi kufikia kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Amina Salum na Januari Makamba, waligombea urais wa Tanzania na John Magufuli, Edward Lowassa na Bernard Membe (wote watatu ni marehemu) mwaka 2015.

Balozi Amina anasema, licha ya Mzee Mwinyi kufanya mabadiliko ya uchumi lakini alikuwa na mchango mkubwa katika kuwainua wanawake kiuongozi, tena akiwapa nafasi ambazo wengi waliamini zinashikiliwa na wanaume pekee.

Katika uongozi wake alikuwa na imani kubwa na wanawake katika kubadilisha sura ya nchi, jamii na familia na katika baraza lake la mawaziri aliwachagua wanawake kadhaa na kuwapa wizara za kuziongoza.

"Miongoni mwa wanawake hao ni mimi Amina, Mzee Mwinyi akiniteua kuwa Naibu Waziri wa Fedha na akiwa na imani kubwa na wanawake na akipenda waonyesha vipawa na uwezo wao," anasema Balozi Amina.

Aidha, wengine waliopata nafasi katika baraza lake la mawaziri ni Fatma Said Ali, Gertrude Mongella na Anna Makinda na wote hao alifanya kazi nao kikamilifu, akisema kwa mara ya kwanza aliteuliwa kwenye wadhifa huo mwaka 1995 na baadaye kumpa nafasi ya Waziri wa Mambo ya Nje.

"Mzee Mwinyi aliniamini kunipa nafasi ya uongozi katika Wizara ya Fedha nikiwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo, ni mtu ambaye akikupa kazi anakuamini na aliponipa nafasi aliniambia nakupa jukumu hili kwa sababu ninaimani utaweza," anasema Balozi Amina.



Balozi Amina Salum Ali



Fatma Baraka maarufu. Bi Kidude.

ALIMWONYA URAIS

"Alinipa wosia wakati aliponiteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje, ikiwamo kusoma, kuwasikiliza watu na kukitafuta kizuri chenye maslahi na nchi na si vinginevyo." Anasema.

"Mzee Mwinyi kanisaidia sana hadi kufikia hapa na kila nilipokuwa nagombea nafasi za uongozi nikienda kumuona na kutaka ushauri kwake alinishauri bila ya kunivunja moyo," anakumbusha.

Aidha, anasema alipogombea umakamu mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake CCM (UWT) na alimshauri kuwa akagombee na kumpa baraka zake hadi aliposhinda.

Kadhalika anasema wakati alipogombea nafasi ya urais wa Zanzibar mwaka 2000 alimfata na kumweleza lengo lake hilo ili kupata ushauri na baraka zake lakini alimweleza kuwa siyo kama hawezi lakini hilo bado gumu kutokana na itikadi za Watanzania.

"Hata nilipogombea urais wa Jamhuri ya Muungano aliniambia nenda kagombee kidogo kidogo watafahamu. Hakuna aliyepata ulezi wa Mzee Mwinyi na kufanikiwa kama mimi sikatai nadhani watakuwa wapo wengine wengine kwani alikuwa mlezi wetu bora," anasema Balozi Amina.

Alipokwenda Marekani kuwa balozi, alianza kumuona na kumuaga na aliendelea kumsisitiza kusoma na kuzifahamu sera za Amerika na Tanzania na kumpa baraka zote katika safari yake hiyo.

"Licha ya kuwa Mzee Mwinyi alikuwa mlezi wangu lakini ni mwalimu wa mume wangu alimfundisha Shule ya Bubwini mkoa wa Kakazini Unguja, tunasikitika kuwa ameondoka lakini tunashukuru kuwa tumekaa naye katika umri mrefu wa miaka 98," anasema Balozi, akimsifia pia kwa kukuza Kiswahili.

**KUMWIBUA BI KIDUDE**

Mariyam Hamdani ni mwana mama aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ), anayekumbusha kuwa katika kipindi cha uongozi wa Mzee Mwinyi alifanya juhudi za kuinua sanaa na muziki wa taarab asilia ili inarudi katika heshima yake pamoja na kuwatafuta wasanii wa kuimba nyimbo za Siti Binti Saada.

"Mzee Mwinyi alinitafuta mimi na Fatma Baraka maarufu. Bi Kidude (marehemu) kuziibua nyimbo za gwiji muimbaji na msanii wa Taarab za Siti Binti Saadi marehemu pia na kuinua umaarufu wake ulitikisa Zanzibar zamani," anakumbusha.

Mariyam mwazilishi wa kikundi cha wanawake cha taarabu asilia Zanzibar, anasema katika tasnia ya sanaa Mzee Mwinyi alikuwa mpenzi wa dhati wa taarabu asilia na kasaidia kufufua nyimbo za Siti binti Sadi ambazo wengi sasa wanazifahamu na kama asiweka juhudi hizo watu wasingezijua zingekuwa zimeshapotea.

Anasema ili nyimbo hizo kuendelezwa alimtafuta Bi Kidude aliyetembea dunia nzima kuitangaza Zanzibar kutokana na nia yake ya kuendeleza taarabu asilia yenye nyimbo kadhaa kwa mfano 'Muhogo wa Jang'ombe, Ya Laiti na Ungurusumbwe.'

Aidha, anasema Mzee Mwinyi ni muumini halisi wa taarabu asilia na aliwainua wasanii wanawake wa taarab hiyo lakini pia alisaidia kuikuza lugha ya Kiswahili.





# CAMARTEC yaanzisha kiwanda darasa cha kubangua korosho

Na Allan Isack, aliyekuwa SINGIDA

KUTOKANA na wakulima wa korosho kukumbana na kero ya walanguzi wa zao hilo, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), kimeanzisha kiwanda darasa cha kubangua korosho katika Wilaya ya Manyoni mkoani Singida.

Akizungumza jana na baada ya Bodi ya CAMARTEC kutembelea kiwanda hicho, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof.Valerian Silayo, alisema kiwanda hicho, kimeanzishwa kwa lengo la kuwasaidia wakulima wasiuze korosho ghafi badala yake waongeze thamani korosho zao.

"Lengo la kuanzishwa kwa kiwanda hiki darasa ni kuhakikisha wakulima wanasaidika kubangua zao hilo, badala ya kuuza likiwa ghafi kwa walanguzi hao kwa kuwa wamekuwa wakiwanyonya kwa muda mrefu," alisema.

Alieleza kuwa wakulima wakiongeza thamani ya zao hilo, itawasaidia kuuza kwa bei ya juu ambapo itakuwa chachu ya kuinua sekta ya kilimo hasa kwenye kilimo cha korosho. Prof. Silayo katika hatua nyingine aliipongeza Halmashauri ya Manyoni kwa kutoa eneo la ujenzi wa kiwanda hicho, pamoja na kulinda miundombinu ya kiwanda kitakwenda kuwa mkombozi kwa wakulima wa zao hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa CAMARTEC, Paythias Ntella, alisema kiwanda darasa kitatoa fursa kwa wakulima kujifunza teknolojia za kubangua korosho sambamba na vijana kujifunza kutumia teknolojia hizo, ili kutengeneza kipato kwa kuongeza thamani ya zao la korosho.

Aidha, Ntella aliishukuru serikali pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuwezesha ujenzi huo ambao utakwenda kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya kilimo.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Charles Mchembe, aliwataka wakulima wa korosho kuchangamkia fursa ya kujipatia teknolojia zilizoko katika kiwanda hicho ili ziwasaidie kubangua korosho zao.

Meneja wa Tawi la Bodi ya Korosho wilayani humo, Ray Mtangi, alikishukuru kituo hicho kwa jitihada za kuanzisha kiwanda katikati ya mashamba makubwa ya korosho.

Alisema wakulima wamesogezewa huduma za ubanguaji wa korosho karibu hivyo zitasaidia kupunguza uuzaji wa korosho ghafi kwa masoko ya ndani na nje ya nchi.

**Wakulima wamesogezewa huduma za ubanguaji karibu hivyo zitasaidia kupunguza uuzaji wa korosho ghafi kwa masoko ya ndani na nje ya nchi.**

# Waziri Gwajima afafanua dhana ya usawa wa kijinsia

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema suala la usawa wa kijinsia si dhana ya kupoka madaraka ya wanaume ya asili kwenda kwa wanawake.

Akizungumza jana jijini hapa katika kikao kazi cha utekelezaji wa progamu ya kizazi chenye usawa kwa Wakurugenzi wa Sera na Mipango, Dk. Gwajima alisema suala hilo limekuwa mtihani kwa jamii na kila mtu anatoa tafsiri yake na kwamba wamejipanga kutoa elimu katika jicho la maendeleo ya kawaida ya jamii.

"Kumekuwa na upotoshaji, nimeongea na Waziri wa Habari na Teknolojia ya Mawasiliano, Nape Nnauye, twende kwenye mijadala huko hewani wanakojadili na kupotosha ili dhana ya usawa wa kijinsia ieleweke, wajue katika jukwaa la kizazi chenye usawa kuna maeneo mengi," alisema.

Alisema mwaka 2021 ulifanyika mkutano wa Kimataifa wa Jukwaa la Kizazi chenye usawa uliofanyika jijini Paris Ufaransa ambapo Tanzania iliwasilisha ahadi za nchi kupitia Rais Samia Suluhu Hassan kuwa kinara katika katika utekelezaji wa eneo la pili kuhusu haki na usawa wa kiuchumi.

"Rais wetu katika kuwapenda sana Watanzania aliona haki na usawa wa kiuchumi ni tatizo unamilikiwa zaidi na jinsia ya kiume na ya kike kuachwa, ndipo matatizo yanapoanzia ukiangalia nafasi ya mwanamke katika maendeleo na ustawi wa jamii tunapata mabaya na madhira mengi, hivyo tuweke mazingira ya kuzifanya hizi jinsia mbili ziwe sawa katika haki na usawa wa kiuchumi," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatuma Toufiq, alisema Bunge litaendelea kuishauri serikali namna bora ya utekelezaji wa jukwaa la kizazi chenye usawa.

"Itakapofikia suala la bajeti tutashauri serikali iweze kupatikana bajeti ya kutosha kwa kuwa nchi yetu imekuwa kinara kwenye haki za usawa kiuchumi tutakapokwenda kuripoti tuoneshe namna Rais wetu alivyokinara na mambo tuliyoyafanya," alisema.



Mkazi wa Utemini, Manispaa ya Singida, Sanje Damiani (51), anayeteseka kwa maumivu ya mifupa kukakamaa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aomba msaada kuokoa maisha dhidi ya maradhi yanayomwandama

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

MKAZI wa Utemini Manispaa ya Singida, Sanje Damiani (51) ambaye anateseka kwa maumivu ya mifupa kwa takribani miaka 40, anawaomba wasamaria wema kumsaidia fedha itakayogharamia bima ya afya, ili akamilishe vipimo hospitalini.

Sanje ambaye kwa sasa anasumbuliwa zaidi na tatizo la kukakamaa mshipa mkubwa wa shingo linalomfanya ashindwe hata kuigeuza, uvimbe shingoni na mwili kukosa nguvu, amesema anaamini akipata bima atapata matibabu ambayo yatampa nafuu kubwa na kupona.

Alisema anaamini akipona ataweza kujishughulisha na kupata kipato kuliko sasa ambapo miaka mitatu anaishi kwa kutegemea huruma ya wasamalia wema.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Sanje alisema licha ya kusumbuliwa na maradhi mbalimbali tangu akiwa na umri wa miaka tisa, yaliyopelekea baadhi ya viungo vya mikono na miguu kufa ganzi hilo halikumfanya ashindwe kujifunza ushonaji nguo uliokuwa ukimwingiza kipato tangu alipofika umri wa kuanza kujitegemea.

Alisema ni miaka mitatu imepita tangu uvimbe ulipomwanza shingoni kwa nje baadaye akapatwa na tatizo la kukohoa mfululizo na hatimaye uvimbe huo uliingia ndani ambapo tatizo la kukakamaa mishipa ya shingo likajitokeza na kumkalisha chini.

Sanje mama wa watoto wawili ambao wote hawajaanza kujitegemea alisema alikwenda katika sehemu kadhaa za kutolea huduma za afya, ikiwamo Hospitali ya Rufani ya Mkoa Singida na Benjamin Mkapa Dodoma, lakini alishindwa kufanyiwa uchunguzi wa kina wa matatizo hayo kwa kushindwa kugharamia vipimo.

Alibainisha kuwa kwa ujumla kwa sasa anahitaji msaada wa matibabu, chakula na mahitaji mengine ya kibinadamu huku akiwashukuru baadhi ya ndugu zake ambao walimsaidia zaidi kipindi cha mwanzo wakati changamoto hizo zinamwanza.

Kwa yeyote atakayeguswa kumsaidia kwa namna yoyote, anaweza kuwasiliana naye kwa namba yake ya simu ya mkononi, ***0762- 931063***.





# Jamii yaaswa kutembelea wafungwa nyakati zote

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATANZANIA wameshauriwa kuwa na utamaduni wa kuwatembelea wafungwa waliofungwa kwenye magereza mbalimbali na kuwasaidia mahitaji muhimu wakati wote badala ya kusubiri siku za matukio maalumu pekee.

Aidha, wananchi wametakiwa kuondokana na hofu ya kutembelea wafungwa magerezani kwa maelezo kuwa ni mahali salama ambapo mtu yeyote anaweza kutembelea na kuwasaidia wafungwa kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Msaidizi wa Mkuu wa Gereza la Ruanda jijini Mbeya upande wa wanawake Mrakibu Msaidizi wa Magereza, Enea Mwaisemba wakati akipokea mahitaji ya wafungwa wanawake yaliyotolewa na wadau.

Wadau waliotoa misaada hiyo ni Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Sauti ya Mama Afrika kwa kushirikiana na Taasisi ya Twende Pamoja ambazo zinashughulikia mambo mbalimbali ya kijamii mkoani Mbeya.

Mwaisemba alisema licha ya jitihada za serikali kuhakikisha wafungwa wanapata huduma zote, lakini wanahitaji ushirikiano kutoka kwa jamii kusaidia mahitaji mengine kwa wafungwa hao hasa wanawake kwa kuwa wanao uhitaji mkubwa.

"Nawashukuru sana kwa kuleta mahitaji haya, niwaombe tusisubiri wakati wa sikukuu na matukio maalumu tu ndipo tulete msaada gerezani, watu wetu wanayo mahitaji wakati wote hivyo kila mnapofanikiwa njooni mara kwa mara," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Sauti ya Mama Afrika, Tabitha Bugali, alisema wameshirikiana na Taasisi ya Twende pamoja Foundation kutoa vitu vyenye thamani ya zaidi ya Sh. 480,000, ikiwa ni sehemu ya kuwapa faraja wafungwa wanawake kuelekea kilele cha Siku ya Mwanamke Duniani Machi 8.

Alisema wametoa mahitaji mbalimbali ikiwamo taulo za kike, sabuni, mafuta ya kupaka, miswaki, dawa za meno pamoja na mavazi ili kuwasitiri wanawake wenzao.

Aliwataka wadau na taasisi zingine za kijamii kushirikiana na serikali kuwasaidia wafungwa hao akieleza kuwa gerezani ni sehemu ya kurekebisha tabia na siyo sehemu ya mateso kama ambavyo wengi wamekuwa wakifikiri.

"Tumeona tujumuike na wenzetu kuwapa faraja ili wasione kama wameadhibiwa, kwa sababu kwa sasa tunajua magereza ni chuo cha mafunzo ili wanapotoka hapa wakawe raia wema," alisema Tabitha.

Hata hivyo alisema wataendelea kuwatembelea wafungwa hao pamoja na makundi mbalimbali ya kijamii wakiwamo watoto yatima kwa lengo la kuyafariji.

Machi 8 ya kila mwaka wanawake nchini wanaungana na wenzao duniani kote kuadhimisha siku yao kwa lengo la kutetea haki zao na kuhamasishana kuchangamkia fursa mbalimbali zikiwamo kuwania nafasi za uongozi serikalini.

# Afariki dunia kwa kusombwa na maji akivuka mto

**Na Mwandishi Wetu,** WANGING'OMBE

MWANAMKE mmoja Esther Mkeleza (70) mkazi wa kijiji cha Wangutwa Kata ya Uhambule wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe amefariki dunia kwa kusombwa na maji wakati akivuka mto.

Tukio hilo lilitokea Februari 29, mwaka huu majira ya jioni ambapo mwanamke huyo alikuwa akienda kwenye shughuli zake.

Akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe, Claudia Kitta, alisema wananchi wanapaswa kuepuka kujaribu kuvuka mito inayopitisha maji kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha kwani usalama unakuwa ni mdogo.

Aliongeza kuwa, "Hili kwa sasa ni tukio la pili la wananchi kufariki, mwezi wa kumi mwaka jana, mwanamke mmoja akiwa na mtoto wake mgongoni alifariki dunia wakati akijaribu kuvuka mto uliokuwa umejaa maji, hivyo nisisitize wananchi waepuka kujaribu kuvuka mito yenye maji mengi," alisema Kitta.

Kwa upande wa wakazi wa Kata ya Uhambule walisema mvua hivi sasa ni nyingi hivyo wamepokea maelekezo ya mkuu wa wilaya.



Baadhi ya wachimbaji wadogo wa madini katika eneo la Makongorosi Kijiji cha Majimoto, Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, wakiwa katika eneo hilo juzi wakiomba walipwe fidia ndipo wapishe uwekezaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waomba elimu lishe kukabili udumavu kwa watoto

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI Halmashauri ya Mji Njombe mkoani Njombe, wameomba serikali kuendelea kutoa elimu ya lishe bora, ili kukabiliana na udumavu kwa watoto.

Wakizungumza na Nipashe wamesema kulingana na kubanwa na majukumu mengi wanashindwa kutekeleza jukumu ka malezi, lakini serikali isisitishe juhudi za kutoa elimu.

Mmoja wa mkazi wa Mtaa wa Sido, Ester Mlelwa, alisema majukumu ya kiuchumi yanawafanya kushindwa kufuta taratibu za malezi.

"Ni vile tunakuwa bize katika kutafuta riziki, kupata chochote kwa ajili ya familia kwa sababu baadhi ya kinababa ni wavivu kufanya kazi, majukumu yote ya nyumbani wanatuachia sisi ikiwamo kusomesha watoto," alisema Mlelwa.

Alisema kuwa ili mtoto apate malezi pamoja na lishe bora ni lazima kinababa washiriki.

Frola Kalinga alisema tatizo kubwa la watoto kuwa na utapiamlo na udumavu unatokana na wazazi kushindwa kuzingatia mlo kamili.

"Utamaduni nao unachangia maana unakuta tumezoea kula makande lakini wakiendelea kutuelimisha basi tutabadilika," alisema Kalinga.

Kwa upande wa Basilius Mligo alikiri kukabiliwa na majukumu makubwa hususani za ujasiriamali.

Katibu Tawala Wilaya ya Njombe, Agatha Mhaiki, aliwataka watendaji wa kata kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu ya lishe bora kwa wananchi ili kufanikisha kampeni ya kupunguza udumavu wilayani humo.

"Nasisitiza kwa watendaji wote wa kata kwenda kuhamasisha viongozi wote wa vijiji na mitaa kutoa elimu ya lishe, kwa kuanda mikutano mbalimbali ya elimu kuhusu lishe kwa vitendo juu ya kuandaa mlo kamili kwa watoto pamoja na umuhimu wa kuzingatia lishe yenye mchanganyiko wa makundi yote ya vyakula," alisema Mhaiki.

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji Njombe, Fransisca Mosha, alisema kutokana na juhudi ambazo wamekuwa wakizifanya za kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya lishe wameweza kuwafikia wazazi wa watoto wenye umri wa miezi 0 hadi 23.



# Wanahabari watakiwa kuelimisha jamii masuala ya kifedha, kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

VYOMBO vya habari vimetakiwa kuwa mstari wa mbele kuainisha changamoto za kiuchumi na kifedha zinazoikabili jamii ili zipatiwe ufumbuzi na taasisi za kifedha.

Akizungumza mwishoni mwa wiki visiwani humo katika kikao maalum na uongozi wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC), Meneja wa Biashara wa Benki ya CRDB Zanzibar, Abdalla Duchi, alisema kuna changamoto ya uhaba wa elimu ya kifedha katika jamii jambo linalopelekea kuzorota kwa shughuli za maendeleo.

Alisema kuwa pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhimiza ujasiriamali na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, bado elimu jumuishi ya kifedha inahitajika ili kuwe na matokeo chanya.

Aidha, Duchi aliahidi kuendelea kutumia vyombo vya habari na waandishi wa habari kueleza shughuli zinazofanywa na benki hiyo, hivyo aliwataka wanahabari kuendelea kushirikiana nao kusambaza elimu kwa umma.

"Niwapongeze kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kuelimisha jamii juu ya masuala yanayohusu ustawi wao kiuchumi na kijamii jambo linalopaswa kufanywa kwa kasi zaidi kwa mashirikiano tunayoyaanzisha leo," alieleza Duchi.

Alisema kuwa benki hiyo ina huduma zinazowagusa wananchi wa ngazi zote ikiwamo akaunti ya kiislamu Al Barakah na bima mbalimbali zinazoweza kuwanufaisha wateja pindi wanapopatwa na majanga, misiba au ulemavu.

"Miongoni mwa bidhaa tulizonazo ni bima ya mtu mmoja mmoja na ya vikundi ambayo hutoa mafao yasiyopungua Sh. milioni moja kwa ajali, kifo, majanga, ulemavu wa kudumu, elimu na kadhalika kwa gharama inayoanzia shilingi 1,000", alieleza meneja huyo.

Mwenyekiti wa ZPC, Abdallah Mfaume, alisema lengo la ziara hiyo inayofanyika kila mwanzo wa mwaka ni kuimarisha mahusiano baina ya klabu na wadau wake.

Alisema kuwa ZPC ni taasisi na mwamvuli wa waandishi wa habari wanaoishi na kufanya kazi katika vyombo mbalimbali vya habari vya ndani na nje ya Zanzibar, ikiwa na jukumu la kuwaunganisha kitaaluma ili kujenga weledi wanachama wake kupitia shughuli mbalimbali.

Aliongeza kuwa katika kutekeleza majukumu yake, ZPC hutoa mafunzo yanayowajengea uwezo wanachama wake na waandishi wa habari hivyo kukua kwa mahusiano baina yake na benki hiyo kutaongeza uelewa wa jamii na wanachama wa klabu juu ya masuala ya kifedha na njia za kujiongezea kipato.

"Tumekuwa na utaratibu huu kila mwaka lengo ni kukumbushana juu ya namna bora ya kufanya kazi pamoja kwa malengo ya kukuza ufanisi wa malengo tuliyojiwekea kupitia shughuli za taasisi zetu," alisema Mfaume.

Meneja Biashara wa Benki ya Kiislamu wa CRDB Zanzibar, Anwar Said, alisema amefurahishwa na ziara ya viongozi hao na kuongeza kuwa benki hiyo inaendelea kutoa huduma kupitia akaunti ya Al Barakah toka ilipoanzishwa mwezi Novemba 2021.

"Katika benki ya kiislamu kuna huduma na bidhaa nyingi sana ikilinganishwa na benki nyingine ambazo tutahitaji msaada wa vyombo vya habari kuujulisha umma," alieleza Anwar.



Waziri wa Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Canada, Arif Virani (kushoto), akizungumza kwenye kituo cha huduma za sheria Zanzibar alipotembelea kituo hicho jana. Kulia ni Mwenyekiti wa Kituo cha Huduma za Sheria, Prof. Cris Maina Peter na wa pili kulia ni Balozi wa Canada nchini, Kyle Nunas. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## Wizara yaita wananchi kuchanja mbwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDARA ya Maendeleo ya Mifugo Zanzibar imesema sababu inayopelekea uwepo wa mbwa wanaozurura ovyo mitaani visiwani humo ni kutokana na uwepo wa majalala ya taka.

Hayo yalisemwa na Daktari Mkuu wa wanyama katika idara hiyo, Dk. Ali Zahran Mohamed, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu chanjo ya kichaa cha mbwa visiwani humo, alisema ongezeko la wanyama hao na kueleza kuwa wanakosa tiba ya chanjo kwa wakati kutokana na kutokuwa na wamiliki.

Alisema kwa mwaka huu idara yake imeendesha zoezi la uchanjaji na mbwa wapatao 3,616 walipatiwa huduma hiyo katika wilaya zote kisiwa cha Unguja.

Dk. Ali alisema idara hiyo ilijipanga vyema kufikia malengo yake kwa asilimia 100, lakini kutokana na uwepo wa mbwa wazururaji kuwakosa wamefikia asilimia 90.6 katika chanjo hiyo.

Aidha, alisema katika utoaji wa chanjo hizo bado wanaendelea kutoa chanjo bure kwa kila mwaka ili kuepusha athari za kichaa cha mbwa kujitokeza na kuathiri wengine sambamba na kumwathiri binadamu.

Alisema kuwa kuna haja kwa wananchi wanaofuga mbwa kupeleka wanyama wao wakapate chanjo kwa vile idara inachukua juhudi ya kuhakikisha mbwa wote wanapewa chanjo kwa kiasi kikubwa ili kupunguza madhara.

Mkuu wa Kitengo cha Tiba na Ufuatiliaji wa Mifugo, Asha Ibrahim Khator, alizitaja dalili za mbwa mwenye kichaa ni pamoja na kutokwa mate mara kwa mara, kuogopa maji na mwangaza, kukimbia bila sababu yoyote na kubweka sana.

Mfugaji kutoka Kiombamvua Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, Issa Abdallah Salum, aliishukuru Idara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mashirikiano waliyompatia katika utoaji wa chanjo kwa wanyama wake na kuiomba idara hiyo kuwapatia elimu wafugaji wengine wanaopuuza uchanjaji wa mbwa wao.

# Serikali yajipanga kuimarisha ujenzi laini mpya za umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaib Hassan Kaduara, amesema serikali imejipanga kuimarisha ujenzi wa laini mpya za umeme katika maeneo yote yakiwamo ya uwekezaji.

Kaduara aliyasema hayo jana wakati akikagua kazi za ujenzi wa laini hiyo na kuzifanyia marekebisho, laini zinazosababisha uwepo wa umeme mdogo katika maeneo ya Mtoni Unguja.

Alisema hatua hiyo ni mkakati wa serikali katika kuimarisha huduma bora kwa wananchi na kueleza kuwa tayari vifaa vipya vinaendelea kufungwa katika maeneo mbalimbali vyenye gharama kubwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa huduma hiyo inapatikana kama ilivyokusudiwa.

"Tunajua kuwa kuna malalamiko mengi ya wananchi juu ya tatizo la kuzima umeme mara kwa mara hii inasababishwa na baadhi ya miundombinu yetu kuwa chakavu na kuzidiwa lakini hatufurahi kuona watu wanaendelea kuteseka," alisema Kaduara.

Aidha, alisema ukiachilia mbali marekebisho hayo, hivi sasa wanampango wa kujenga laini ya Kilo Volt 132 kutoka Welezo kwenda Bambi, kutoka Bambi kwenda Makunduchi na kutoka Bambi kwenda Nungwi ikiwa ni sehemu moja wapo ya uwekezaji.

Meneja Uendeshaji wa ZECO, Mohamed Zubeir Kombo, aliwataka wananchi kuwa wastahimilivu katika kipindi hiki cha kufanyiwa matengenezo miundombinu hiyo.

"Matengenezo haya tunamatumaini makubwa yatafanyika kwa uhakika na wananchi wataweza kufurahia huduma zetu bila kuwapo usumbufu wa aina yoyote," alisema.

Katika maboresho hayo yanayoendelea kufanyika katika kituo cha Mtoni, baadhi ya maeneo yanatarajiwa kukosa umeme yakiwamo yanayotumia laini mpya ya Kaskazini inayohusisha maeneo ya Bumbwini, Mangapwani, Fujoni, Mahonda, Kinyasaini, Chaani, Kiwengwa, Pwani Mchangani na Matemwe.

Aidha kwa upande wa laini kongwe ya Fumba, maeneo yatakayoathirika ni pamoja na Kilimahewa, Magogoni, Mwanakwerekwe Ijitimai, Taveta Kwarara, Kiembesamaki, Tomondo, Kisauni, Kombeni, Nyamanzi, Dimani, Bweleo na Fumba.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**REBECA JULIUS MKUNDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1491/0044** kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia SHANGANI SECONDARY SCHOOL mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIG/29419/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SALUM SALEHE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3502/0249/2013** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia OYSTERBAY SECONDARY SCHOOL MWAKA 2013 na cheti cha DIPLOMA chenye namba ya usajili **NS 3502/0249/2013** kilichotolewa na **NACTE** kupitia **MACHAME HEALTH TRAINING INSTITUTE** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIG/29306/2024**

## TANGAZO

Mimi **GERRY JOEL KAKIZIBA** namtangazia aliyeacha **Tela (Trailer)** la kubebea mizigo aje kulichukua hapa kwangu jirani na **JKT KUNDUCHI** kuanzia leo tarehe 5-3-2024 mwisho tarehe 10-3-2024.

Nambari ya simu: **0713527285**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA OFA YA KIWANJA

**Sospenous Robart Mabele** mkazi wa Manispaa ya Shinyanga anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja **Namba 377 Kitalu "PP"** eneo la **Mwadui Manispaa ya Shinyanga,** Ofa hiyo ilipotea maeneo ya Shinyanga kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha polisi kilichopo karibu au ofisi ya ardhi au awasiliane na Sospenous Mabele kwa Simu Namba **0767935855.** Taarifa hii imeripotiwa Kituo cha Polisi Shinyanga na kupewa **PHQ/SHI/SHI/629/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA SHINYANGA LILILOPO SHINYANGA**

**SHAURI LA ARDHI NA.56 LA 2023**

**SOSOMA NDALAHWA KIDAGO ................................MDAI**
**(Msimamizi wa mirathi ya marehemu Masele Ndalahwa Kidago)**

**DHIDI YA**

**GWIYEYA NGUMIJI ........................................MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: GWIYEYA NGUMIJI**
**POPOTE ULIPO:**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi tajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako katika Baraza la Ardhi na nyumba la Wilaya ya Shinyanga. Shauri hilo limepangwa kutajwa tarehe 19/03/2024 saa 2:30 asubuhi katika baraza hili . Hivyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili siku hiyo wewe mwenyewe au Wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu shauri hilo. Pia unaelekezwa kwamba hati ya madai ipo Barazani na unaweza kuifuata ili uweze kujibu dai hilo .

**FAHAMU KWAMBA:** Kushindwa kufika Barazani litasikiliza shauri hilo na kutolea uamuzi bila wewe kuwepo. Ofisi za Baraza zipo mkabala na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga

**IMETOLEWA:** na mimi kwa AMRI na CHAPA ya Baraza leo tarehe 15.02.2024

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) SHINYANGA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANI WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**SHINYANGA**

**MAOMBI MADOGO YA MADAI NAMBA 10 NA 28 YA MWAKA 2023**

**EMMANUEL MADUHU MBITI ..............................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**1. MWANTIMBA VILLAGE & 7 OTHERS ...............WAJIBU MAOMBI**
**2. MALI MCHENYA, 3. BUHULU TULANDULA, 4. SHOTO KIDUMU**
**5. PIMBI BUHULA, 6. BOYA SAMSONI, 7. BARIADI DISTRICT COUNCIL**
**8. ATTORNEY GENERAL**

**KUITWA SHAURINI**

**POPOTE ULIPO**
**MALI MCHENYA,BUHULU TUNDALA,SHOTO KIDUMU,PIMBI BUHULA,BOYA SAMSONI,BARIADI DISTRICT COUNCIL,ATTORNEY GENERAL NA MWANTIMBA VILLAGE&7 OTHERS**

Hii ni kukupa taarifa kuwa, Mleta maombi amefungua shauri la maombi madogo ya madai tajwa hapo juu dhidi yako. Maombi hayo yamepangwa kusikilizwa tarehe 11/3/2024 saa 5:00 asubuhi mbele ya Mhe.Jaji F.H.MAHIMBALI.

Hivyo unaamriwa Kuhudhuria siku hiyo bila kukosa na kama hutohudhuria maombi hayo yatasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na lakiri ya Mahakama hii leo tarehe 29/1/2024.

**WARSHA S.NG"HUMBU**
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANAIA**
**KANDA YA SHINYANGA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA MAHALI DODOMA**

**MAOMBI NA. 214 YA MWAKA 2023**

**EDWARD MNYAMAGOLA ..........................................MDAI**

**DHIDI YA**

**JULIUS NGANGA**
**KABURA**
**NAOMI OMARY**
**ANDREW MATARAGIO.......................................... WADAIWA**

**KWA:**
**JULIUS NGANGA, KABURA, NAOMI OMARY, ANDREW MATARAGIO**
**POPOTE WALIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili nyinyi binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 27.03. 2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa ajili ya kusomewa maoni ya Wazee wa Baraza na Hukumu.

**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa mmepokea hati ya Wito, Baraza litaendelea na utaratibu wa kisheria.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 01 ya mwezi Machi, 2024.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA TANZANIA

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA INAYOKETI SUMBAWANGA**

**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA. 142 YA 2021**

**MAYUNGA JACKSON MAGIGI AND 289 OTHERS......WARUFANI**

**DHIDI YA**

**JV OF 15G NEW CENTURY COMPANY LIMITED......MRUFANIWA**

**KWA:**
**MANAGING DIRECTOR,**
**JV OF 15G NEW CENTURY COMPANY LIMITED**

**POPOTE ULIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la Rufaa ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Sumbawanga tarehe 13/03/2024 saa tatu kamili asubuhi(3:00).

Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hutahudhuria wewe binafsi au mwakilishi walo anaetambulika kisheria basi rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wako.

Imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 28/02/2024

A. L. KALEGEYA
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA YA RUFANI**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF BUNDA DISTRICT AT BUNDA**

**PROBATE AND ADMINISTRATICN CAUSE NO 3750 OF 2024**

**IN THE MATTEROF THE ESTATE OF THE LATE VICENT BAHAME BENEDICTOR**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTTERS OF ADMINISTRATICN OF ESTATE BY BUNDALA JOSEPH ISAMBAJA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to came and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.

The matter cames for mention ot the 22 day of March 2024 before B.C.Sokanya(SRM)

Dated at BUNDA this 26th day of February 2024

DISTRICT COURT TANZANIA

HON. ..............................
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
BUNDA.

---


**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARIKIMATAIFA

## HALI YA HATARI YATANGAZWA;

# Wafungwa 100 wasalia gerezani, 4,000 watoroka

**Port-au-Prince, HAITI**

MAELFU ya wafungwa wametoroka Gereza la Taifa la Haiti, lililoko katika mji mkuu. Inakadiriwa wafungwa 4,000 hawamo gerezani na takribani 90 wakisalia.

Kulikuwa na makabiliano ya bunduki usiku wa kuamkia juzi, kati ya polisi wa kitaifa na makundi yenye silaha, baada ya tukio hilo.

Serikali yatangaza hali ya hatari na sheria ya kutotoka nje usiku katika mji huo na hali hiyo inapaswa kudumu angalau saa 72.

Waziri Mkuu wa Haiti, Ariel Henry, yuko nje ya nchi. Alienda wiki iliyopita nchini Kenya, kusaini makubaliano ya pande mbili hizo, kuruhusu maofisa 1,000 wa polisi wa Kenya kuongoza kikosi cha usalama cha kimataifa.

Umoja wa Mataifa (UN), uliidhinisha kikosi hicho kusaidia Haiti, kupambana na vurugu za makundi yenye silaha na kurejesha usalama. Haikuwa wazi alikokuwa waziri huyo mkuu siku ya Jumapili, juzi.

Ofisi ya Rais wa Kenya, William Ruto, haikujibu ombi la VOA la habari kuhusu mahali alipo Henry.

Serikali ya Henry, haijatoa taarifa rasmi kuhusu kinachoendelea Haiti. Ubalozi wa Marekani nchini Haiti, bado haujatoa maoni yoyote hadharani kuhusu vurugu za mwishoni mwa wiki.

Waandishi wa habari wa VOA waliokwenda kwenye gereza hilo, katikati mwa mji mkuu wa Port-au-Prince na waliona miili ndani na nje ya jengo hilo.

Mhandisi, ambaye hakutaka jina lake litajwe kwa sababu hakuwa amepewa ruhusa ya kuzungumza kwa niaba ya maofisa wa usalama, alisema alikuwa akifanya kazi na polisi wa kitaifa kufanya tathmini ya hali Jumapili asubuhi.

Taarifa kutoka eneo la tukio zilidai kwamba, wafungwa 99 walibakia ndani ya gereza. Alisema gereza hilo awali lilikuwa na karibu wafungwa 4,000. Vimetangazwa vifo vya watu 12.

***VOA***



Hali ya machafuko inayoshuhudiwa kila kukicha nchini Haiti, kwenye maeneo tofauti ya mji mkuu wa nchi hiyo, Port-au-Prince. **PICHA: DW**

# Somalia rasmi mwanachama jumuiya A. Mashariki

**Arusha, TANZANIA**

SOMALIA rasmi imekuwa mwanachama kamili wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), baada ya kukamilisha hatua zote zinazohitajika.

Ukurasa wa EAC, jana, ulichapisha kwenye matandao wa X kwamba, Somalia imepata uanachama kamili, baada ya kuwasilisha hati yake, ili kuidhinishwa kwa Katibu Mkuu wa jumuiya hiyo.

Chombo cha uidhinishaji ni hati rasmi iliyotolewa na nchi ambayo inakubali kufungwa na mkataba.

Novemba, mwaka jana, wakuu wa nchi nyingine wanachama wa EAC, walikubali kujumuishwa kwa Somalia katika umoja huo.

Somalia inakuwa mwanachama wa nane wa EAC, baada ya Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kenya, Sudan Kusini, Tanzania, Rwanda na Uganda. Hatua hiyo inanuiwa kuimarisha ukuaji wa uchumi nchini humo, ambao bado unaendelea kuimarika kutokana na miongo mitatu ya vita.

***BBC***

# Ghala la chakula la serikali laporwa

**Abuja, NIGERIA**

GHALA la serikali ya Nigeria, limeporwa huku kukiwa na mzozo wa chakula. Polisi katika mji mkuu wa Nigeria, Abuja, wamewakamata watu 15.

Nchi hiyo inakabiliana na mzozo wa gharama ya maisha, kituo cha utangazaji cha kibinafsi cha Channels TV, kimeripoti.

Maofisa wa usalama walitumwa kwenye ghala la kuhifadhia chakula lililoko katika eneo la Tasha, jijini humo, baada ya kundi la watu kupora juzi.

Magunia 26 ya mahindi, pikipiki tano na baadhi ya paa za aluminiam, zilizoharibiwa zilipatikana kutoka kwa washukiwa, polisi walisema.

Wakala wa Kitaifa wa Usimamizi wa Dharura (NEMA), umeimarisha ulinzi katika maduka yake kote nchini, kufuatia tukio la uporaji.

Kufutwa kwa ruzuku ya mafuta Mei, 2023, kumechochea mfumuko wa bei na kuongeza gharama ya maisha na kusababisha maandamano ya hivi karibuni katika majimbo kadhaa ya Nigeria.

Mgogoro wa kiuchumi unaendelea, licha ya serikali kuunda kamati ya kudhibiti bei za vyakula na kuamuru kutolewa kwa akiba ya chakula.

Benki ya Maendeleo ya Afrika (BOA), imeonya kuwa nchi hiyo inaweza kukumbwa na machafuko ya kijamii kutokana na gharama kubwa ya maisha.

***BBC***

**Magunia 26 ya mahindi, pikipiki tano na baadhi ya paa za aluminiam, zilizoharibiwa zilipatikana kutoka kwa washukiwa, polisi walisema.**

# Balozi wa Ujerumani Moscow aitwa kujieleza

**Moscow, RUSSIA**

WIZARA ya Mambo ya Nje ya Russia, ilimwita jana, Balozi wa Ujerumani mjini Moscow, kujieleza baada ya kuvujishwa kwa nyaraka za siri za jeshi la Ujerumani, kuhusu Ukraine.

Shirika la habari linalomilikiwa na serikali ya Russia, RIA Novosti, liliripoti jana, kwamba balozi huyo alifika katika Wizara ya Mambo ya Nje ya Russia mjini Moscow, akiitwa kuhusiana na mazungumzo yaliyovujishwa ya maofisa wa Ujerumani, kuhusu vita nchini Ukraine. Taarifa hiyo ilisema, Balozi Alexander Graf Lambsdorff, aliwasili katika wizara hiyo jana, asubuhi, bila kutoa maoni yoyote kwa waandishi wa habari.

Rekodi ya sauti ya dakika 38 ya mazungumzo kati ya maofisa wa jeshi la Ujerumani, ilichapishwa jioni, Ijumaa, kwenye mitandao ya kijamii ya Urusi.

Maofisa hao walikuwa wakijadili uwezekano wa kutumwa nchini Ukraine kwa makombora ya Taurus, yaliyotengenezwa Ujerumani na athari zake.

Na mada nyingine zilizojadiliwa na maofisa hao wa Ujerumani, ni pamoja na kulenga makombora kwenye daraja muhimu juu ya mlango wa bahari wa Kerch, unaounganisha Russia na Crimea, jimbo ambalo lilitwaliwa na Russia, mnamo 2014.

Serikali ya Russia, ilisema kwamba nyaraka hizo za siri zilizovujishwa zinaonyesha ushiriki wa moja kwa moja wa nchi za Magharibi katika mzozo wa Ukraine.

Msemaji wa Kremlin, Dmitry Peskov, alisema haikuwa wazi kama jeshi la Ujerumani, Bundeswehr, walikuwa wanachukua hatua kama mpango wao wenyewe au ilikuwa ni sehemu ya sera ya serikali.

***DW***

# 'MNAOENDA ALL-AFRICA GAMES FANYENI KAMA SIMBA, YANGA'

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, amezitaka timu zinazoenda kuipeperusha Bendera ya Tanzania katika michuano ya All-Africa Games, kuhakikisha wanafuata nyayo za Klabu za Simba na Yanga ambazo zimeiheshimisha nchi kwa zote kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema timu hizo zimeiheshimisha nchi kwa kuweka rekodi msimu huu ya kuwa taifa pekee katika bara hili kupeleka timu mbili kwa msimu mmoja katika hatua ya robo fainali jambo ambalo ni mara ya kwanza kwa zote mbili kwa pamoja kutinga hatua hiyo.

Hata hivyo, kwa Simba hii ni mara ya tano inatinga hatua hiyo kwenye michuano hiyo wakati kwa Yanga ikiwa ni mara ya kwanza.

Ndumbaro alitoa kauli hiyo juzi usiku katika hafla ya kuwaaga na kuwakabidhi bendera ya Tanzania wanamichezo wanaokwenda kuliwakilisha taifa katika michezo ya All-Africa Games ya 2024, inayofanyika Accra nchini Ghana kuanzia Machi 8 hadi 23, mwaka huu.

Ndumbaro alisema taifa linamatarajio makubwa sana na timu zinazowakilisha nchini katika michuano hiyo kutokana na maandalizi bora waliyoyapata kuelekea katika mashindano hayo.

"Ninafahamu Tanzania itashiriki katika jumla ya michezo saba ambayo ni kriket, ngumi za wazi, ridhaa, kuogelea, soka la wanawake, judo na baskeli, hii michezo inafanya jumla ya wanamichezo (wachezaji na wataalamu) wote wanaounda timu ya Tanzania kufika 75. Idadi hii ni kubwa na ni kwa mara ya kwanza Tanzania inapeleka wanamichezo wengi kiasi hiki kwenye michezo hii ya Afrika.

"Ni jambo zuri na la kujivunia, hatutakiwi kushiriki tu, nendeni mkapambane na kuliletea heshima taifa, muwe kama Simba na Yanga ambao wameweka historia ya kuingia robo fainali katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa kwa pamoja msimu huu," alisema Ndumbaro.

Aliongeza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari wa mbele kuiwezesha michezo, hivyo wasimwangushe, bali waende kupambana na kuleta heshima kwenye michuano hiyo ya All-Africa Games.

"Ni imani yangu kuwa wote tunafahamu kwanza michezo ya All-Africa Games ni mikubwa sana barani Afrika ambayo inahusisha nchini zote za bara hili. Kimsingi hii ndio Olimpiki yetu hapa Afrika. Timu zimekuwa kwenye kambi za mazoezi kwa zaidi ya mwezi mmoja zikijifua kikamilifu kwa ajili ya kwenda Ghana, si tu kushiriki bali kupambana na kuendeleza rekodi ambayo wameifanya Simba na Yanga hapa nchini kwa mwaka huu," alisema Ndumbaro.

Timu ya Soka la Wanawake U-20 (Tanzanite) wameondoka jana ambao wamepangwa Kundi A, pamoja na Ghana, Uganda na Ethiopia. Wanamichezo wengine wanatarajiwa kuondoka Jumamosi wiki hii.

Katika hatua nyingine Waziri Ndumbaro ametoa maagizo kwa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kusitisha malipo yote kwa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta).

Dk. Ndumbaro alisema amekasirishwa na maneno ya Katibu Mkuu wa Chaneta, Rose Mkisi, kusema kuwa serikali hawajali mchezo huo zaidi ya kuwekeza katika soka.

"Nawaagiza BMT kumuita Katibu wa Chaneta katika kamati ya nidhamu, pia aje na ushahidi wa tuhuma alizozisema katika mahojiano na chombo (kimoja)cha habari.

"Sitisha malipo yote hasa yale ya Afrika Kusini ambayo mlilipia tiketi, pia katika mkutano ambao nitafanya hivi karibuni kwa kukutana na vyama na mashirikisho wasiwepo hadi hili tatizo liishe," alisema waziri huyo.

## Singida mechi 8 bila ushindi Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

HALI ni mbaya kwa timu ya Singida Fountain Gate kwani baada ya kipigo cha mabao 2-0 Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, dhidi ya Mtibwa Sugar, imefikisha mechi ya nane kucheza bila kupata ushindi wowote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Timu hiyo ambayo ilipata pigo la kutimkiwa na wachezaji wake nyota kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo kama kina Joash Onyango, Duke Abuya, Elvis Rupia, Marouf Tchakei na wengine waliotimkia Ihefu, imeteremka hadi nafasi ya nane ya msimamo ikiwa na pointi 21 kwa michezo 19 iliyocheza mpaka sasa, kutoka nafasi ya nne ilipokuwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

Mara ya mwisho kushinda ilikuwa ni Novemba 27, mwaka jana, ilipoifunga Coastal Union mabao 2-1 nyumbani, na hadi leo hii haijaonja ladha ya ushindi ikicheza idadi hiyo ya mechi.

Katika michezo minane iliyocheza bila ushindi, imepoteza mechi tano na kutoka sare mara tatu.

Rekodi zinaonyesha kuwa, Desemba Mosi, mwaka jana, ikiwa nyumbani, Uwanja wa Liti, Singida ambapo kwa sasa imehama kwenda Mwanza, ikitumia Uwanja wa CCM Kirumba, ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya JKT Tanzania, na sare nyingine na nyumbani ilikuwa Desemba 11 ikitoka suluhu dhidi ya KMC, kabla ya kwenda kukutana na kipigo cha bao 1-0, Uwanja wa Nyankumbu, Geita, dhidi ya Geita Gold, Desemba 21, mwaka jana.

Timu hiyo ikaenda mkoani Kagera na kukutana na kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar, mechi iliyochezwa Februari 12, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, na siku tatu baadaye ikapata kipigo kingine cha mabao 3-1 dhidi ya Prisons, Uwanja wa Sokoine Mbeya, kabla ya kwenda kuambulia sare ya bao 1-1, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora, dhidi ya Tabora United.

Baada ya hapo ilikwenda CCM Kirumba na kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Azam, mchezo uliochezwa Februari 22, mwaka huu kabla ya Jumamosi iliyopita kubamizwa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar.

**MMETUNYOSHA...**



Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha (kushoto), akipongezwa na wa Jwaneng Galaxy, Morena Ramoreboli, baada ya kuiongoza timu yake kuwatembezea kichapo kikali cha mabao 6-0, kwenye mechi ya kuhitimisha hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tabora United yapata ushindi wa kwanza 2024

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Timu ya Tabora United, juzi ilifanikiwa kupata ushindi wake wa kwanza mwaka huu, baada ya kuifunga Coastal Union bao 1-0, katika mchezo wa raundi ya 19 ya Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora.

Timu hiyo ilikuwa haijapata ushindi wowote tangu Desemba Mosi, mwaka jana, ilipoifunga Mtibwa Sugar mabao 2-1, kwenye uwanja huo, lakini baada ya hapo ikacheza mechi nane bila kupata ushindi, ikifungwa nne na sare nne.

Bao pekee lililomaliza rekodi mbaya ya Tabora United, liliwekwa wavuni na Andy Bikoko dakika ya tatu ya mchezo na mpira ukachezwa kwa dakika 87 zilizosalia bila bao.

Ushindi huo umeisogeza timu hiyo hadi nafasi ya tisa ya msimamo, ikifikisha pointi 21 kwa michezo 19 iliyocheza.

Kocha wa timu hiyo, Goran Kopunovic, alisema anawashukuru wachezaji wake kwa kujituma na kupata ushindi kwani walikuwa wanacheza mechi kwa presha.

"Tumeshinda, sasa tunataka kuwa na mwendelezo wa hili ambalo tumelifanya leo," alisema.

Rekodi zinaonyesha kuwa baada ya ushindi dhidi ya Mtibwa, ilitoka sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Mashujaa, Desemba 5, ikachapwa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Ihefu, Desemba 8, kabla ya kudunguliwa bao 1-0 na Yanga, Desemba 23, Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, ikiwa ni mechi ya mwisho kwa mwaka jana.

Mwaka huu ilikutana na kipigo cha mabao 4-0 nyumbani dhidi ya Simba, Februari 6, sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo ikicheza nyumbani, Februari 11, suluhu dhidi ya Azam FC, Februari 10, sare ya bao 1-1 dhidi ya Singida Fountain Gate, Februari 25, na kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Prisons, Februari 28, mwaka huu.

Kipigo cha bao 1-0 ilichokipata Coastal Union nacho kinakuwa cha kwanza mwaka huu kwao kwani mara ya mwisho ilipoteza mechi ya ligi, Novemba 27, mwaka jana, ilipochapwa mabao 2-1 dhidi ya Singida Fountain Gate, na baada ya hapo ilicheza mechi sita, ikishinda tano na sare moja.

Imebaki kwenye nafasi ya nne na pointi zake 26 kwa michezo 18 iliyocheza mpaka sasa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SARGENT AFIKIRIA BRENFORD
KLABU ya Brentford inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Norwich na Marekani, Josh Sargent mwenye umri wa miaka 24, huku wakijiandaa kwa ajili ya kuondoka kwa mshambuliaji wa England, Ivan Toney (27), ambaye anazivutia Chelsea na Arsenal. ***(Football.London)***

### ROBERTSON MKATABA MPYA
LIVERPOOL inatazamiwa kuanza mazungumzo na Andy Robertson kuhusu mkataba mpya msimu huu wa majira ya joto na hawana wasiwasi na ripoti zinazomhusisha mlinzi huyo wa kushoto na Bayern Munich, mwenye umri wa miaka 29. ***(Football Insider)***

### CAMARDA AFUATILIWA CITY
KLABU za Manchester City na Borussia Dortmund zinamfuatilia mshambuliaji wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Italia chini ya umri wa miaka 17, Francesco Camarda, ambaye anatazamiwa kukataa ofa ya mkataba wa kulipwa katika klabu hiyo ya Serie A atakapofikisha umri wa miaka 16 wiki ijayo. ***(Gazzetta dello Sport via Football Italia)***

### GYOKERES KIPAUMBELE ARSENAL
MSIMU huu Arsenal imempa kipaumbele mshambuliaji wa Sporting Lisbon na Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 25. (***TodoFichajes)***

### KVARATSKHELIA KUBAKI NAPOLI
BABA wa Khvicha Kvaratskhelia amesema winga huyo wa Georgia mwenye umri wa miaka 23, atabakia Napoli msimu huu wa majira ya joto licha ya kuhusishwa na Real Madrid na Barcelona. ***(Radio Serie A via Deportivo)***

### KIPAUMBELE CHA RABIOT
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, anatazamia kuyapa kipaumbele mazungumzo ya mkataba mpya na Juventus kuhusu uwezekano wa kuondoka katika klabu hiyo ya Serie A, huku Tottenham Hotspur ikimfuatilia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 wakati huu wakitafuta kusajili kiungo wa kati. ***(CaughtOffside)***

### GUTIERREZ ATAKIWA ARSENAL
ARSENAL inajiandaa kupambana na Manchester United katika kinyang'anyiro cha kumsajili mlinzi wa Hispania, Miguel Gutierrez, kutoka Girona mwenye umri wa miaka 22. ***(Fichajes)***

### FILAMU YA KLOPP LIVER
LIVERPOOL inatarajia kutengeneza zaidi ya pauni milioni 10 kutokana na filamu ya 'fly-on-the-wall', inayoangazia msimu wa kuagwa kwa Jurgen Klopp. ***(Sun)***

### RAMSDALE ATAKIWA MILAN
AC Milan wanamfuatilia mlinda mlango wa Arsenal na England, Aaron Ramsdale mwenye umri wa miaka 25, kama mbadala wa kipa Mfaransa Mike Maignan mwenye miaka 28. ***(Ekrem Konur)***

### BILIC NA IRELAND
KOCHA wa zamani wa West Ham, Slaven Bilic, hayumo kwenye kinyang'anyiro cha kuwania nafasi ya kuinoa Jamhuri ya Ireland licha ya Mcroatia huyo ambaye kwa sasa anainoa Klabu ya Al-Fateh ya Saudi Arabia kuhusishwa na jukumu hilo. ***(Irish Independent)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CASEMIRO: MAN UNITED IITUMIE CITY KAMA KIOO

●●●Historia ya klabu hii inajieleza yenyewe, lakini leo kila mtu anataka kuwa kama Man City...

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Casemiro amesema kwamba wamiliki wapya wa klabu hiyo wenye hisa chache wanapaswa kuitumia Manchester City kama „kioo" katika jitihada zao za kuirejesha timu hiyo kileleni mwa soka la Uingereza.

United ilifungwa na Man City mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Etihad Jumapili, licha ya Marcus Rashford kufunga bao la mapema.

Ilikuwa ni mechi ya kwanza ya Manchester dabi tangu dau la Sir Jim Ratcliffe la kuinunua klabu hiyo ya Old Trafford kuthibitishwa, na Casemiro akatoa ukumbusho mkali wa pengo kati ya timu hizo mbili.

Alipoulizwa kama anaona dalili chanya kutoka kwa kundi jipya la umiliki wa hisa chache na kama kuna safari ndefu kwa United kuifika City, Casemiro aliiambia ESPN Brasil: „Hilo ndilo lengo kubwa, pia tunapaswa kuwa wanyenyekevu kukubali kwamba kwa sasa ndio wakati wao. Historia ya Manchester United inajieleza yenyewe, lakini leo kila mtu anataka kuwa kama Man City.

"Tuna kioo hapa, ambacho ni Man City, na wamekuwa wakifanya kazi nzuri."

Ratcliffe, mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kemikali ya INEOS, ameahidi "kuirudisha timu kwenye kileleni chake" ndani ya miaka mitatu.

Kuna matumaini kwamba kuwasili kwa bilionea huyo wa England mwenye umri wa miaka 71, kutachochea kuibuka tena baada ya zaidi ya miaka 10 bila taji - kipindi ambacho City wameshinda Ligi Kuu mara sita.

"Bila shaka, watu kutoka nje wanapofika, ambao wanataka kuongeza na kuboresha kiwango cha klabu, ni muhimu kila mara," alisema Casemiro.

"Ni wazi kwamba Kampuni ya INEOS na wamiliki wapya wanataka kufanya hivi. Natumaini wamiliki wapya watafika na kukua pamoja nasi, kwani ni muhimu kwa klabu kuwa na watu wanaotaka kukua hapa."

United walichukua uongozi dhidi ya City kutokana na bao la kustaajabisha la Rashford, lakini mambo yakawabadilikia kipindi cha pili.

Kikosi cha Pep Guardiola kilifanikiwa kupiga mashuti 27 langoni ikilinganishwa na matatu kutoka kwa United, lakini baadaye Erik ten Hag alidai kuwa matokeo hayakuonyesha kuwa kuna pengo kubwa kati ya timu hizo mbili.

"Hapana, sifikirii hivyo," alisema Hag kocha wa Man United.

"Unaweza kuona tuna matatizo mengi ya majeruhi na bado tulikuwa na nafasi. Kweli tungeweza kufunga bao la pili."

# DE JONG, PEDRI WAIPA PANCHA BARCELONA

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA inakabiliwa na tatizo la majeruhi katika safu ya kiungo baada ya Frenkie de Jong na Pedri kulazimishwa kutolewa nje katika kipindi cha kwanza cha sare ya Jumapili kwenye La-Liga dhidi ya Athletic Club katika Uwanja wa San Mames.

De Jong alitolewa nje kwa machela dakika ya 26 baada ya kutua vibaya chini na kuumia kifundo cha mguu. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uholanzi alikaa nje ya uwanja kwa miezi miwili mwanzoni mwa msimu huu kutokana na kuteguka kifundo cha mguu.

Naye Pedri alitolewa nje kabla ya mapumziko akiwa na jeraha lake la tatu la misuli kwenye kampeni hii. Tatizo la misuli ya paja lilimfanya kuwa nje kwa miezi miwili Agosti na alikosa wiki tatu mwanzoni mwa mwaka kutokana na tatizo lingine la misuli.

Wachezaji wote wawili jana Jumatatu walifanyiwa vipimo, lakini Kocha wa Barca, Xavi Hernandez, alisema hajajua kiwango walichoumia.

"Majeraha yaliathiri timu kwa sababu Frenkie na Pedri ni wachezaji wawili muhimu kwa jinsi tunavyotaka kucheza," alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Pedri amekuwa akija vizuri tena baada ya jeraha lake la mwisho, amefanya mazoezi vizuri sana wiki hii. Frenkie, pia. Anahusika sana katika uchezaji wetu. Ni hasara mbili kubwa.

"Haionekani vizuri. Tumewakosa leo (juzi) na tutawakosa. Tunatumai ni kwa muda mfupi."

Mechi dhidi ya Athletic ilisha kwa suluhu, ikiwaacha Barca pale walipoanza siku: katika nafasi ya tatu kwa pointi 58, nane nyuma ya vinara wa LaLiga, Real Madrid.




## Gakpo: Kutua Liver ulikuwa uamuzi bora

**LIVERPOOL, England**

CODY Gakpo amefichua kuwa alifanya mazungumzo na Manchester United kuhusu uhamisho wa msimu wa majira ya joto wa 2022, lakini kuhamia kwake Liverpool msimu wa baridi mwaka uliofuata ulikuwa "uamuzi bora kwangu."

Mshambuliaji huyo mwenye uwezo mwingi alifurahia miaka mitano katika kikosi cha kwanza cha PSV Eindhoven kabla ya kusajiliwa na 'Wekundu' hao Januari 2023.

Wakati wa majira ya joto ya kwanza ya Erik ten Hag kuinoa United, Gakpo alifanya mazungumzo naye kuhusu kuhamia Old Trafford, lakini hatimaye makubaliano hayakuweza kukamilika.

Gakpo alibaki PSV hadi dirisha la majira ya baridi na kisha akajiunga na Liverpool kwa dau la awali la pauni milioni 35.4.

Katika mahojiano na Sky Sports, Gakpo alifunguka juu ya ukubwa wa mazungumzo haya ya uhamisho na United na jinsi ilivyokuwa bora kwake kubaki na kusubiri kutua Liverpool.

"Ilikuwa majira ya joto kabla ya kujiunga na Liverpool. Nilikuwa nikiwasiliana na klabu (United) na kocha - yeye ni Mholanzi kwa hivyo nilizungumza naye pia," alisema Gakpo.

"Mwisho wa siku ilishindikana, na wakati wa majira ya baridi Liverpool ilikuja. Ulikuwa uamuzi bora kwangu."




## Bayern Munich yakomaa na Davies

**MUNICH, Ujerumani**

MKURUGENZI Mtendaji wa Bayern Munich, Jan-Christian Dreesen, amekiri klabu hiyo ipo kwenye mazungumzo ya kina na Alphonso Davies kuhusu mustakabali wake huku kukiwa na nia kutoka Real Madrid.

Mkataba wa sasa wa Davies pale kwenye dimba la Allianz Arena unamalizika 2025, na hivi karibuni The Athletic iliripoti kwamba amekubali kwa mdomo kujiunga na Madrid msimu huu wa majira ya joto au ujao.

Mpango ni kumleta beki huyo wa kushoto kabla ya msimu wa 2024/25, lakini kama ada haiwezi kuafikiwa na Bayern, basi Madrid watamsajili kwa uhamisho wa bure mwaka unaofuata.

Hata hivyo, Bayern wameweka wazi kuwa hawataki kumpoteza Davies bure na wanatarajia ama kumfunga kwa mkataba mpya au kumuuza msimu huu wa majira ya joto.



Bayern ilithibitisha kuteuliwa kwa Max Eberl kama mkurugenzi mpya wa michezo wiki hii, na Mkurugenzi Mtendaji, Dreesen amefichua kuwa klabu hiyo inaweza kufanya harakati nyingine ya kuongeza mkataba wa Davies.

"Kwa Alphonso tuna mchezaji ambaye amekua vema kwenye winga ya kushoto, si tu kwa sababu ya kasi yake, lakini pia kwa sababu ya tabia yake na uwelevu wake katika miaka ya hivi karibuni," alisema Dreesen.

"Tunazungumza na wakala wake (kuhusu mustakabali wake). Tutaona jinsi ilivyo ngumu. Max Eberl sasa ataingilia kati mkataba huo. Christoph Freund (mkurugenzi wa michezo), tayari amezungumza kuhusu hilo. Lakini sehemu ya ujenzi mpya wa kikosi na nyongeza ni kuangalia picha kuu, na hiyo inategemea jinsi Max na Christoph wanavyoona siku zijazo."

Katika utambulisho wake wiki hii, Eberl alisema kuhusu Davies: "Jan-Christian na Christoph wamekuwa na majadiliano. Nitajaribu kuendeleza mazungumzo. Hakuna klabu inayotaka kupoteza wachezaji bure. Ni lazima nione jinsi hali ilivyo."

# YANGA YAZIVUTIA KASI IHEFU, AZAM

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kikosi cha Yanga kimeingia kambini kujiandaa na mechi zinazofuata za Ligi Kuu, zikiwamo dhidi ya Ihefu FC na Azam FC.

Meneja wa timu hiyo, Walter Harrison amesema kwa sasa wamesahau kila kitu, akili yao ipo katika mechi nne mfululizo ambazo watacheza kuanzia Ijumaa ijayo dhidi ya Namungo FC, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi, lakini pia wana mechi ngumu dhidi ya Ihefu FC na Azam FC.

"Kwa sasa Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, akili yake ni kuwaandaa vijana kwa ajili ya mchezo wa Ijumaa dhidi ya Namungo, na tunakuwa na mechi nne mfululizo, kwani Machi 11 tutakuwa nyumbani kuikaribisha Ihefu, Machi 14 tutacheza dhidi ya Geita Gold hapa hapa nyumbani, tarehe 17 Machi tutakuwa Azam Complex kucheza dhidi ya Azam FC, ni mechi ngumu na zipo karibu karibu, hivyo inahitaji umakini na maandalizi mazuri," alisema Harrison.

Yanga imekuwa ikipata upinzani mkali inapocheza dhidi ya Ihefu FC hasa inapocheza ugenini kwani katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliangukia pua kwa kichapo cha mabao 2-1, mechi iliyochezwa, Oktoba 4, mwaka jana katika Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya, lakini kwa sasa imehamia Singida.

Hata hivyo, mechi hiyo itachezwa jijini Dar es Salaam, ambapo angalau hupata unafuu.

Pamoja na kupata matokeo mazuri mara kwa mara dhidi ya Azam, lakini pia hupata upinzani mkali, huku mechi baina yao ikizalisha mabao mengi kwa kila timu.

Mara ya mwisho zilipokutana katika mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, Oktoba 23, mwaka jana, Yanga ilipata ushindi wa mabao 3-2.

Wakati meneja huyo akisema hayo, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema licha ya kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, hawatoidharau timu yoyote ile watakayokwenda kucheza nayo, wala Ligi Kuu yenyewe.

"Nawaambia mashabiki na wanachama wetu, pamoja na kwamba tumetinga hatua ya robo fainali na sasa bado tupo kwenye furaha, lakini sasa akili yetu tuipeleke kwenye mechi za Ligi Kuu.

Kuanzia wachezaji, viongozi, benchi la ufundi na mashabiki, akili na nguvu zetu tuzielekeze huku kwa sababu ni muhimu sana.

Ni muhimu sana, tunaanza na Namungo Ijumaa, kwa hiyo ni lazima tuwekeze nguvu zetu hapo tuweze kufanya vizuri, kwa sababu huku ndiko kunatupa nafasi na tiketi ya kucheza mechi za kimataifa, bila ya kupata nafasi za juu huku kwenye ligi huwezi kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, hatuidharau timu wala ligi yenyewe," alisema Kamwe.

Aliongeza kuwa hata kama timu ikitwaa ubingwa wa Afrika, lakini kama haikupata nafasi kwenye ligi yake ya nyumbani msimu ujao haiwezi kushiriki na hilo linawafanya wawe makini zaidi kwa sasa katika mechi hizo.

Yanga ambayo ndiyo bingwa mtetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, pia ni vinara wakiongoza wakiwa na pointi 43 sawa na Azam FC kwa sasa, lakini wako pungufu kwa michezo mitatu.

Inaongoza kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa, ikiwa imecheza mechi 16, Azam ikifikisha michezo 19 mpaka sasa.

## BUSU LA 3-1...



Kiungo mshambuliaji wa Manchester City, Phil Foden, akimpongeza kwa busu, straika wa timu hiyo, Erling Haaland, baada ya kuifungia timu yao bao la tatu ikiwa ni baada ya yeye kutupia mawili wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Manchester United kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Etihad juzi usiku. **PICHA: MTANDAO**

# KenGold njia nyeupe kukwea Ligi Kuu Bara

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya KenGold imejiwekea mazingira mazuri ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, baada ya Jumamosi kuifunga Biashara United mabao 2-1, katika mechi kali ya Raundi ya 23 ya Ligi ya Championship, iliyokuwa ikisubiriwa kwa hamu na mashabiki wengi, ikichezwa Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

Biashara United ndiyo timu iliyoonekana kuleta upinzani mkali kwa KenGold kwani zilikuwa zimeachana kwa pointi moja, huku kila timu ikishinda mechi mfululizo, hivyo ushindi huo umeonekana kuwa ahueni kwa vijana hao wa Mbeya.

Ushindi huo umeifanya KenGold kufikisha pointi 53 na kuiacha Biashara United, ikibaki nafasi ya pili ikiwa na pointi 49.

Timu zote sasa zimebakiwa na mechi saba ili kumaliza ligi hiyo, KenGold ikionekana kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kupanda moja kwa moja.

Vinara hao wameshinda mechi 16, sare tano na kupoteza mbili tu mpaka sasa, huku Biashara ikishinda mechi 15, sare nne na imepoteza mechi ya nne katika mchezo huo.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo, timu ya Mbuni FC ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Maafande wa Trasit Champ katika mchezo uliochezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Matokeo hayo yanaifanya Mbuni kufikisha pointi 40 na kupanda hadi nafasi ya sita, ikisaka nafasi ya angalau kucheza mechi za mchujo katika kusaka timu ya tatu itakayopanda Ligi Kuu msimu ujao.

Kipigo hicho kimeifanya Transit Camp kubakiwa nafasi ya 13 na pointi zake 20, ikiwa kwenye eneo hatarishi la uwezekano wa kushuka daraja na kwenda ‚First League' msimu ujao.

## Fei Toto, Azizi Ki vitani Ligi Kuu

INATOKA UK. 24

wa Februari, ninaimani nikiendelea kufuata maelekezo ya benchi la ufundi mbona hizo tuzo za uchezaji bora wa mwezi zitakuja sana kwangu," alisema Fei Toto.

Kuhusu ubingwa, kiungo huyo alisema wanaimani ya kufanya vizuri katika michezo iliyosalia huku wapinzani wao wakifanya vibaya baadhi ya michezo wanaweza kutwaa taji hilo.

"Kama tutaendelea kwa ubora huu na kuonyesha ubora tuliokuwa nao katika mechi zilizopita kwenye mechi zijazo, tunaimani kubwa ya kufanikisha hayo malengo yanayotarajiwa na mashabiki wetu," alisema kiungo huyo.

Azam FC wako nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kucheza michezo 19 na kujikusanyia pointi 43 sawa na Yanga iliyopo kileleni, lakini yenyewe ikiwa imecheza michezo 16 huku Simba katika nafasi ya tatu pointi 36 ikicheza mechi 15.

## Benchikha ataka moto CAF Ligi Kuu

INATOKA UK. 24

ionyeshwa na wachezaji wangu ninaamini tutakuja kuona katika mechi zijazo na kuitumia michezo hiyo ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya mechi za robo fainali," alisema Benchikha.

Aliongeza kuwa anafanya kazi hatua kwa hatua, na kwamba amemalizana na Jwaneng Galaxy kwa kufanikiwa kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na sasa wanahitaji kutafuta pointi 12 mwezi huu wa Machi.

Mshambuliaji wa Simba, Pa Omar Jobe, alisema mpira ni kujiamini na kujiamini kile unachokifanya, na matarajio yake ni kupambania timu yake kufikia malengo yanayotarajiwa.

"Mashabiki wanatakiwa kuniamini, nitapambana na kuendelea kufuata maelekezo ya benchi la ufundi na kushirikiana na wachezaji wenzangu kufikia kile ambacho kinatarajiwa na Wanasimba," alisema Jobe.



Benchikha

Michezo
Jumanne Machi 5, 2024
Nipashe

De Jong, Pedri waipa pancha Barcelona UKURASA 22




# FEI TOTO, AZIZI KI VITANI LIGI KUU

●●●Kiungo huyo wa Azam FC amemtangazia vita mbio za kiatu baada ya kumfunika kwa...




**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kutimiza idadi ya mabao 11 ya kufunga kwenye Ligi Kuu msimu huu, kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', ametangaza kula sahani moja na kinara wa kufumania nyavu wa Yanga, Stephen Aziz Ki, katika mbio za kuwania kiatu cha ufungaji bora.

Fei Toto juzi alifanikiwa kufunga mabao mawili wakati wakishinda 4 -1 dhidi ya Dodoma Jiji FC katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, hivyo kufikisha mabao 11 huku akimshusha chini Aziz Ki ambaye ameshacheka na nyavu mara 10 katika ligi hiyo msimu huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Fei Toto alisema amefurahi kuona kila mechi anaisaidia timu yake kupata matokeo mazuri na ataendelea kupambana kuona Azam FC inakuwa katika nafasi nzuri kwenye ligi.

Alisema kwa sasa mipango yake ni kuisaidia timu kupata matokeo mazuri ambayo ni mwisho wa msimu kuona wanafikia malengo yao kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao.

"Kwa sasa nahangaikia timu yangu katika kupambana na kutafuta matokeo mazuri, kuhusu ufungaji bora hilo jambo lipo, nitaendelea kupambana na kufuata maelekezo ya mwalimu. Aziz Ki ni mchezaji mzuri anajua kufunga, lakini tutapambana naye.

"Nafurahi kuwa mchezaji bora

INAENDELEA UK. 23

# Benchikha ataka moto CAF Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutoa kichapo 'kitakatifu' kwa Jwaneng Galaxy ya Botswana kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amewataka wachezaji wake kuweka nguvu na akili zao kuelekea michezo yao minne ndani ya mwezi huu ili, kutafuta pointi 12 na kujiweka vizuri kwenye kinyang'anyiro cha kusaka ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Jumamosi Simba iliibuka na ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, hivyo kufuzu moja kwa moja hatua ya robo fainali, ikiungana na Asec Mimosas ya Ivory Coast ambayo ni kinara wa Kundi lao la B.

Simba ilitoa kipigo hicho ikitoka kuwaadhibu TRA ya Kilimanjaro kwa ushindi kama huo kwenye mechi ya Kombe la FA.

Hata hivyo, sasa Benchikha amewataka wachezaji wake kugeuzia akili zao kwenye mechi za Ligi Kuu Bara huku akisema lengo lake ni kutaka kuona timu yake inaendelea kuwa na ubora ambao wamekuwa nao katika michezo miwili iliyopita kwa kutafuta pointi katika mechi tatu za nyumbani na moja ya ugenini.

Simba inakabiliwa na kibarua kigumu cha kutafuta pointi hizo kuanzia Machi 6, 12 na 15, ambapo watacheza dhidi ya Tanzania Prisons, Singida Fountain Gate FC na Mashujaa FC mechi hizo watakazocheza nyumbani Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro huku Machi 9, mwaka huu wakishuka Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga dhidi ya Coastal Union.

Akizungumza na Nipashe jana, Benchikha alisema hawana muda wa kupoteza kwani wanakibarua kigumu cha kuendelea kusaka pointi katika mechi za ligi kwa kufanikisha malengo yao ya kutwaa ubingwa.

Alisema wamekuwa na ratiba ngumu, lakini wamefanikiwa kuvuna alama kwa ubora walionyesha mechi zilizopita kwenda kuonyesha katika mchezo unaofuata wa Ligi Kuu.

"Tumecheza vizuri sana katika michezo ya nyuma, ubora wa mechi ya juzi ul-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >